Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

لا اله الا الله محمد رسول الله

Mapenzi ya Mungu

DAR ES SALAAM TANZANIA

Toleo Maalum la miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara

JUZU 73 No. 167 | MUHARRAM 1433 AH | DISEMBA 2011 | FATAH 1390 HS | BEI TSH. 500

Tafsiri ya Kurani Tukufu na harakati za uhuru

Ni mwaka 1934, ukoloni ndio umeshika kani, unanuka. Kuna hoteli huwezi kuingia, kosa lako ngozi nyeusi! Shule Fulani huwezi kujiandikisha, kosa lako ngozi nyeusi! Hospitali Fulani marufuku kutibiwa, kosa ni lile lile kwa nini una ngozi nyeusi, nyeusi ja mpingo? Kazi zote zingine hustahili isipokuwa kupiga pasi, shamba boy na sababu yenyewe u mweusi! U mweusi! Kikombe chako cha kunywea maji lazima kiwe tofauti na usiulize ni kwa nini, wewe ni mweusi. Hiyo ndiyo hali aliyoikuta Maulana sheikh Mubarak Ahmad alipoingia Tanganyika mwaka 1934. Giza totoro. Na katika giza hilo nene akatuletea mafundisho tunayoyatolea maelezo hapa chini. Je tutakuwa tumekosea tukisema mafundisho hayo yalisaidia kuleta uhuru wa Tanganyika?



Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad Khalifatul Masih II r.a.

Ilikuwa ni Kurani Tukufu ambayo kwa mara ya kwanza kabisa ilihubiri juu ya uhuru wa binadamu kwa mapana na marefu kiasi hiki ya kwamba dunia ikatoka usingizini, ikawa macho na kuanza kutafuta tunu hii iliyokuwa imepotea. Akina baba na akina mama, wale wa hali ya chini na wale wa hali ya juu kila mmoja akamaizi kuwa uhuru ni haki yake ya kuzaliwa.

Dini ya Islam ilifika katika mwambao wa Afrika ya Mashariki yapata miaka 1000 iliyopita lakini kabla yake hapakuwa na Sheikh yoyote aliyefikiri kwamba kuna haja ya tunu hii kuwekwa katika lugha ya wenyeji – Waswahili. Hivyo hazina zilizomo ndani ya Kurani zikawa ni dhahabu ya kufikirika ya hadithi za Alfu Lelila ul Lela na badala ya kitabu hicho kutumika kwa kumkomboa mwandamu kikawa kinatumika kumtia utumwani kwa kumtisha na kumtumikisha kinyume na mafundisho yake.

Endelea uk. 3

Salamu za Amir Jamaat Tanzania katika kuadhimisha miaka 50 ya uhuru

Ndugu wannachi wapendwa.

Asslaam alaikum warahamtullah wabarakaatuh

Tarehe 9 Disemba ni siku adhimu. Ni siku ya Uhuru.

Tukiwa tunasherehekea siku ya uhuru tarehe 9 mwezi huu wa Disemba 2011, sherehe ya

Endelea uk. 2



Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania

Wanajumuiya ya Ahmadiyya walioshiriki katika harakati za uhuru

Historia ya harakati za uhuru wetu ni ndefu, kuna majina mengi yanayohusishwa na upigania uhuru wa nchi hiyo. Wengi wa wanaotajwa aghalabu huwa ni wale tu waliofanikiwa kuchota madaraka makubwa ya kiserikali baada ya uhuru. Wanakumbukwa kwa mfano Mwalimu J.K. Nyerere, Rais wa kwanza. Rashidi Mfaume Kawawa makamu wa kwanza wa Rais, Bwana John Rupia, Amir Jamal, Sykes, Kaluta Amri Abedi na kadhalika.



Sheikh Kaluta Amri Abedi

Lakini kuna kundi kubwa la watu ambao mchango wao katika madai ya uhuru ulikuwa si jambo la kubezwa, lakini kwa bahati mbaya historia iliwatelekeza, hawakutajwatajwa sana, hivyo hata vizazi vyetu vimekosa kusoma tarehe za watu hao muhimu waliopata kutokea katika nchi hii.

Katika makala hii nimefanya dodosa kuhusu watu wachache ambao ni wafuasi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ambao mchango katika uhuru ulikuwa mkubwa mno, lakini katika kilele cha Mshangao wetu wamekuwa si kitu cha kutajwa katika historia ya uhuru wa nchi yetu.

Jumuiya ya Ahmadiyya kama ilivyo husika na uhuru wa nchi mbalimbali, kama vile Gambia, India, Pakistan

Endelea uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Alhamdulillah

Tanzania Bara yatimiza miaka 50

Mapinduzi ya Kiroho Kwanza

Shukrani zote ni za Allah Aliyejalia nchi yetu tunayoipenda sana ("Kupenda nchi ni sehemu ya imani" -amesema Mtume Mtukufu Muhammad saw) kutimiza nusu karne toka tuiteremshe bendera ya 'Union Jack' ya Mwingereza na kupeperusha bendera yetu tarehe 09/12/1961.

Historia ya uhuru wa Afrika imekuwa na misukosuko, umwagaji damu, mapinduzi, kuibuka kwa utawala wa ki-imra, vita vya wenyewe kwa wenyewe, mauaji, njaa na ukabila.

Hatuwezi kusema tunayo sifa ya pekee sisi Watanzania. Isipokuwa hii ni neema tu ya Mwenyezi Mungu Aliyetujalia kuvuka salama katika wimbi hili kali hadi kujichumia lakabu ya kisiwa cha amani.

Lakini tukumbuke siku zote "Ukiona chombo kinaelea hapana shaka kimeundwa" na uundaji wa chombo unahitaji vifaa, na kifaa kikubwa katika miaka 50 hii ya taifa letu imekuwa ni kutegemea kwetu Mwenyezi Mungu.

Mapambano yetu yaliendeshwa kwa maombi, mikutano ilifunguliwa kwa maombi na saumu zilifungwa. Mwaka 1958 mara baada ya kuisha mkutano maarufu wa Tabora Nyerere alihutubia mkutano wa hadhara mjini humo na neno lake la mwisho lilikuwa 'Mwingereza asipotupa uhuru wetu tutapeleka kesi yetu kwa Mwenyezi Mungu'. Na kweli Mwenyezi Mungu Alisikia kilio chetu.

Uhuru ulipoingia viongozi wetu wakaapa kwa vitabu vitakatifu,

wimbo wetu wa taifa kama sote tunavyofahamu kwamba ni maombi matupu. Bunge letu linafunguliwa na kufungwa kwa maombi. Hii ndio siri kubwa ya mafanikio yetu. Sote kwa umoja wetu tunamtegemea Mwenyezi Mungu.

Tunapoingia katika miaka 50 mingine Inshallah, tunachotaka ili kunusuru nchi yetu ni mapinduzi ya kiroho. Tunachotaka ni kutimiza kwa matendo mafundisho ya dini zetu. Dini zote zinazungumzia kumpenda jirani yako, dini zote zinakaripia wizi na dini zote zinataka tusikaribie zinaa.

Tunatakiwa tusafishe nafsi zetu, likibaki giza kidogo tu litaharibu mwili mzima. Ni mapinduzi ya kiroho kuwafikiria wenzio, kugawana kidogo ulichonacho na wenzio, kuondoa tamaa, kuelewa bila kusahau kwamba sote hapa ni wasafiri na kila kitu tutakiacha. Tusafishe nafsi zetu.

Bila mapinduzi ya kiroho, kilio cha katiba itakuwa ni kazi bure. Na kama wanavyosema 'kutwanga maji kwenye kinu' au kupigia ngoma kwenye maji. Tunahitaji katiba ya nafsi kwanza, nafsi inayoamini kwamba unapokuwa peke yako uelewe Mwenyezi Mungu yupo hapo hapo. Na mnapokuwa wawili Yeye ni wa tatu.

Katika miaka 50 iliyopita kwa kiwango kikubwa sana tumeshughulikia dunia. Si kosa kufanya hivyo, lakini fikra zote, mawazo yote, kutawaliwa na suala la mkate tu si busara kwani nani hajui kuwa binadamu haishi kwa mkate tu?

Huu ni wakati wa viongozi wa dini kulididimiza au kuliokoa taifa hili. Viongozi wa dini watakiwa wawe na tahadhari kubwa. Kuna mahali waliambiwa viongozi hao watakuwa wabaya chini ya ardhi. Fitina itaanza kwao na itawarudia. Kama penye nuru kuna giza bila shaka mahali hapo kuna mushkili. Viongozi wa dini wanatakiwa kuwa mfano na hakuna msiba mkubwa uliokumba bara la Afrika kama kuwa na viongozi wa kidini na kisiasa wanaoamrisha mema na kusahau nafsi zao.

Miaka 50 ijayo Inshallah, tunawataka viongozi wa kidunia na kisiasa wawe ni mfano bora wa uadilifu na wema. Viongozi ambao wanang'ara sio kwa ubingwa na uwezo wa kuzungumza ila kwa kiasi gani wanatekeleza hayo wanayoyahubiri.
Mungu Ibariki Afrika
Mungu Ibariki Tanzania

Mapenzi ya Mungu lilivyosaidia mahubiri

Na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani
Rabwah Pakistan.

Ingawa dini ya Kiislam ilipatikana katika Afrika Mashariki mapema sana lakini mafundisho sahihi ya dini ya Kiislamu yaliletwa na yalifundishwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah. Maana ilikadiriwa hivyo hivyo kwamba Masihi Mau'di na Imam Mahdi aje na aeneze mafundisho sahihi ya dini ya Kiislamu. Masahaba wa Masihi Mau'di walifika katika Afrika Mashariki hasa mijini Mombasa na Zanzibari katika uhai wake. Na mara wakaanza kuhubiri Ujumbe wa Uahmadiyyah.

SHEIKH MUBARAK AHMAD AKAJA

Mnamo mwaka wa 1934 Khalifa Mtukufu wa pili Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. alimtuma Maulana Sheikh Mubarak Ahmad kuwa Mbashiri wa kwanza katika Afrika Mashariki. Alianza kazi ya mahubiri kutoka katika mji wa Nairobi lakini akaona ni afadhali stesheni yake iwe Tabora, kwa hiyo alihamia Tabora. Pamoja na kujifunza Kiswahili alianza kutoa matangazo ya mahubiri.

MAPENZI YA MUNGU YAANZA

Wakati ule Waislamu wa Afrika Mashariki hawakuwa na gazeti lolote la dini kutangazia Neno la Mungu. Maulana Sheikh Mubaraka Ahmad kwa busara yake kubwa alianzisha gazeti la kwanza kabisa la Kiislamu katika Afrika Mashariki kwa jina la MAPENZI YA MUNGU mnamo mwaka 1936. Hata jina la gazeti linaonyesha mapenzi aliyokuwa nayo Sheikh Mubarak Ahmad moyoni mwake kwa Mwenyezi Mungu. Tangu wakati ule gazeti likaendelea hatua kwa hatua katika hali na mazingira tofauti tofauti hadi sasa. Nawapatia wasomaji hongera nyingi sana kwa kutimiza miaka 75 kwa Gazeti letu "Mapenzi ya Mungu".

SURA MPYA YA MAPENZI YA MUNGU

Mnamo mwaka wa 1999 nilipewa usimamizi wa gazeti la Mapenzi ya Mungu kuwa Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah nchini Tanzania. Wakati ule mhariri alikuwa marehemu A.R. Nasibu, Mungu Amsamehe na Ampe Pepo yake. Hatua ya kwanza niliyochukua kwa gazeti, ilikuwa kuhakikishia kwamba gazeti litoke kila Mwezi mfululizo bila kukosa. Kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu tulishinda vizuri katika kupata lengo hili. Kisha tulipangilia kurasa za gazeti kwa mada mbalimbali kama ifuatayo: Malezi na Hotuba za Khalifa Mtukufu, Mahubiri na majibu ya maswali, Matangazo



Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani.
Aliyewahi kuwa Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania

na taarifa ya kazi ya Jumuiya, Shairi na hali ya maendeleo ya nchi.

MAHUBIRI YA MAPENZI YA MUNGU

Kama nitaje mahubiri pekee kupitia MAPENZI YA MUNGU ni ya kutoshelezana kufurahisha sana. Tulikuwa tukitoa mada za mahubiri moja kwa moja, taarifa ya mihadhara na mijadala, na majibu ya maswali. Swali lolote lililotolewa kwa njia yoyote na mtu yeyote wa dini yoyote, lilikuwa jukumu la MAPENZI YA MUNGU kulichimbua na kulijibu barabara. Katika hali hii gazeti moja la Wakristo liitwalo MSEMA KWELI likaanza kuchochea dini tukufu ya Uislamu. Papo hapo MAPENZI YA MUNGU lilikubali kama kawaida yake kutetea dini ya Mungu.

MATOLEO MAWILI KILA MWEZI

Sasa mjadala ulianzia kwa maandishi katika magazeti mawili. MAPENZI YA MUNGU lilikuwa likitoka kila Mwezi ilihali MSEMA KWELI kila wiki. Kwa hiyo kuona shauku ya wasomaji iliamuliwa kwamba MAPENZI YA MUNGU litoke angalau mara mbili kila mwezi ili wasomaji wapate jibu haraka bila kusubiri mwezi mzima. Wasomaji walifurahia sana jambo hili na walimshukuru Mungu kupata matoleo mawili kila Mwezi. Vile vile kurasa za Mapenzi ya Mungu ziliongezwa kuwa kumi.

MKATE MTAMU

Mauzo ya gazeti letu yalizidi sana hata wauzaji magazeti wakaanza kuliuza kwenye vibanda vyao hasa mjini Dar es Salam. Ya kwanza mwl. Omari Mnungu kisha Mwl. Mubaraka M. Abd ur Rahman walisimamia vizuri sana jukumu hili la mauzo mjini Dar. Hata tulipata taarifa kwamba gazeti linauzwa kwenye misikitini mwa madhehebu mengine pia tena kwa bei ya juu. Maana wanunuzi walikuwa zaidi kuliko idadi ya magazeti. Kwa hiyo idadi

Endelea uk. 3

Salamu za Amir Jamaat

Kutoka uk. 1

mwaka huu imezidi uzito wake kwa vile tunamaliza miaka hamsini ya uhuru. Sisi sote tunamshukuru Mwenyezi Mungu Aliyetujaalia na kutuwezesha kuona siku hii adhimu. Huu ni ukweli kwamba uhuru ni neema kubwa sana, na unapatikana baada ya kufanya juhudi kubwa. Na ni kweli kwamba watu wa Afrika walipata uhuru baada ya kufanya jitihada kubwa, lakini pamoja na kupata uhuru kazi haishii hapo, bali majukumu yanaongezeka na kazi inazidi na kazi ile ni ya kuimarisha nchi, kujenga jamii na kudumisha haki na uhuru wa binadamu.

Pamoja na uhuru wa kiutawala ni vyema ieleweke kwamba uhuru kamili wa mwanadamu ni ule unaoletwa na Manabii wa Mwenyezi Mungu, na hivyo mtu hawezi kuwa huru kama hajamjua na kumfuata Nabii wa zama zake.

Basi kila mwanachi na hasa kila Ahmadiyya aweke mbele yake fundisho la Mtume wetu Mtukufu Hadhrat Muhammad s.a.w. kuwa "Kuipenda nchi ni sehemu ya imani" - Afanye jitihada na kutumia mbinu mbalimbali za kuimarisha nchi yetu Tanzania ikiwemo kuufikisha ujumbe wa Islam kwa watu wote.

Mwenyezi Mungu tunakuomba uendeleze amani na utulivu katika nchi yetu Tanzania, bara letu la Afrika na ulimwengu nzima.

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika.
Wasslaam

Tahir Mahmood Chaudhry

Amir na Mbashiri Mkuu

Tafsiri ya Kurani Tukufu na harakati za uhuru

Kutoka uk. 1

Ilikuwa ni Sheikh Mubarak Ahmad wakati ambapo baadhi ya Masheikh walikuwa wakisema ni haramu Kurani Tukufu kutafsiri kwa Kiswahili alipoona haja kubwa ya kuyaweka mafundisho ya Kurani katika lugha ya wenyeji ya Kiswahili.

Tafsiri hii ilichangia na inaendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa juu ya uhuru wa wananchi wa eneo letu hili la Afrika. Kwenye utangulizi wa Tafsiri hiyo ulioandikwa na Khalifa wa Pili Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad ambaye pia alikuwa ndiye Mwalimu wa Sheikh Mubarak imeandikwa:

"Basi, enyi watu wa Afrika ambayo sehemu yake ya mashariki ina lugha ya elimu - Kiswahili, kwa kuweka mbele yenu tafsiri hii naona ladha na furaha, maana katika siku za mwanzo wa Kitabu hiki baralenu liliwalinda wale waliokiamini Kitabu hiki na likakataa kabisa kuwatendea dhuluma na jeuri, bali likakazana kusimamisha adili na haki. Leo mafundisho matakatifu ya Qur'an yako katika hali ya kudhulumiwa kama walivyokuwa wakidhulumiwa walioamini Qur'an.

Kweli Nabii aliyeileta Qur'an Tukufu katika dunia amekwisha kufa, lakini kuwapo kwake kwa kiroho leo kunadhulumiwa zaidi kuliko alivyokuwa miaka 1,400 kabla, alipokuwa akidhulumiwa katika maisha yake ya kimwili. Yeye anasingiziwa, na mafundisho yake yanaelezwa na yanawekwa mbele ya dunia kwa sura mbaya. Na wanaomwamini yeye wanafahamiwa wanyonge na dhalili. Lakini Mwenyezi Mungu anaona ya kuwa hayo si haki. Mtakatifu na mwenye heshima zaidi katika macho ya Mwenyezi Mungu ni Mtume Muhammad s.a.w. ambaye ilimshukia Qur'an hii; na mafundisho yenye haki zaidi ni yale yaliyomo katika Kitabu hiki, yaani Qur'an Tukufu, na ninyi mtayaona wenyewe.

Dunia, katika ghururi na nguvu na uwezo wake, inashughulika kuyapinza mafundisho yake, na inaendelea kuwafedhehesha wanaokiamini Kitabu hiki. Lakini, enyi watu wa Afrika, hata ninyi pia mko katika hali ya namna hii. Wacheni nchi za kigeni, hata katika nchi yenu wenyewe ninyi hamheshimiwi. Hivyo, mafundisho yaliyowapandisha watu miaka elfu moja na mia nne kabla ya leo, waliokuwa washenzi, wasio na maarifa wala elimu, kwenye vilele vya maendeleo ya kila namna ya dunia, lakini yamekuwa katika hali ya kudhulumiwa, na yametiwa umaskini na ufukara - mafundisho haya nayaweka mbele yenu ninyi ambao hali yenu ni ya namna hii hii, nami nawatakieni mkisome Kitabu hiki kwa fikara, na mkitazame kwa macho ya uadilifu na wema ule ule kama alivyofanya mfalme Mwafrika, Najashi, alipowaona Waislamu waliohamia katika nchi yake.

Tena mkitazame kwa akili yenu na busara yenu, wala msiingiwe na athari ya masingizio ya uwongo waliyoleta watu, wala msikitazame kwa miwani ya rangi mbalimbali iliyotengenezwa na watu.

Nina yakini kama mtafanya hivyo, bila shaka mtaijua thamani ya kito hiki kisicho mfano; mtaishika kamba aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu kwa njia ya Kitabu hiki kitakatifu kutoka mbinguni, ili watumishi Wake kwa kuishika wafike Kwake.

Enyi watu wa Afrika! Onyesheni tena dalili ya adili na wema wenu, na toeni msaada kwa kuusimamisha ukweli - ukweli alioutuma Mwumba wenu, Mwenyezi Mungu, ambao pasipo kuukubali mataifa yaliyomo utumwani hayawezi kupata uhuru, na wanaodhulumiwa hawawezi kuokoka katika dhuluma, na wafungwa hawawezi kutoka katika magereza. Nawafikishieni ujumbe wa amani, ustawi na maendeleo. Ujumbe huu si wangu, bali ni ujumbe wa Mwenyezi Mungu ambaye ni Mwumba wenu na Mwumba wangu. Huu ni ujumbe wa Mwenyezi Mungu ambaye ni Mwumba wa mbingu na ardhi. Huu ni ujumbe wa Mwenyezi Mungu ambaye ni Mwumba wa Ulaya na Amerika na Asia.

Njooni. Njooni kwa maelefu. Bali njooni kwa malaki. La bali njooni kwa mamilioni, mkusanyike chini ya bendera ya ukweli, ili sisi sote kwa kuungana pamoja tusimamishe tena ufalme wa Mwenyezi Mungu, na tusimamishe udugu wa wanadamu ulimwenguni, na tusimamishe adili na wema katika dunia.

Mwenyezi Mungu awapeni nguvu na uwezo wa kuitikia wito wangu, nami nipate kuiona siku ambayo ninyi mtasimama pamoja nami bega kwa bega kwa kuendelea na juhudi ya kusimamisha amani na salama, maendeleo na ustawi katika dunia. Na mwishowe juhudi hii ifanikiwe kwa baraka na fadhili za Mwenyezi Mungu".

Nchi za Magharibi zinaweza kujigamba kwa lolote lile, zikidai kwa kujivuna uhuru walionao, lakini ukweli unabaki kuwa uhuru ulioletwa na Islam karne kumi na tatu zilizopita hauna mfano! Ulaya na Marekani hazikuweza kutoa uhuru huo kwa watu weusi, wala Wahindi hawakuweza kutoa uhuru huo kwa wale wanaowaita "wasioguswa". Nchi za Magharibi zinalaani sana utumwa, lakini la ajabu dunia yote imefanywa kuwa watumwa na watu hao wa Magharibi. Mtu hawezi kufikiria mateso makubwa na unyanyasaji mkubwa kuliko ule uliofanywa na unaoendelea kufanyiwa watu weusi na mateso kwa wale wasioguswa wa India. Katika nchi za

Endelea uk. 5



Sheikh Mubarak Ahmad (katikati) akiwa pamoja na Sheikh Amri Abedi kushotoni kwake pamoja na wabashiri wengine wa Ahmadiyya walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kazi ya kutafsiri Kurani Tukufu kwa Kiwahili.

Mapenzi ya Mungu lilivyosaidia mahubiri

Kutoka uk. 2

ya nakala za MAPENZI YA MUNGU ziliongezwa. Kuona hali na shauku hii ya wasomaji marehemu A.R. Nasibu,Mhariri alikuwa akisema kwamba gazeti letu limekuwa mkate mtamu (hot cake) na mahubiri yake yamekuwa kichwa cha mazungumzo nchini (talk of the country). Mapenzi ya Mungu lilikuwa gazeti la pekee lililokuwa likifika na kusomwa mpaka vijiji vya Tanzania na Kenya. Baadhi ya wakati tulikuwa tukipata maoni hata kutoka huko Lamu, Kenya. Tulikuwa na nia ya kutoa MAPENZI YA MUNGU kila wiki ili wasomaji wapate habari moto moto bila kuchelewa lakini wapinzani walitoroka haraka na hawakuweza kusimama kiwanjani.

UKWELI ULIFIKA NA UWONGO ULITOWEKA

Baada ya muda mfupi tu mwandishi wa Msema Kweli sio alinyamaza tu bali alipotea na tuliendelea kumwita na kumsaka kwa majadiliano. Baada ya muda mrefu alijitokeza gazetini mwake kuomba radhi kwamba hawezi kuendelea kujadiliana na Waahmadiyyah, maana amepewa shughuli zingine muhimu zaidi kuliko hiyo na tena alipotea kabisa. Matoleo ya miaka ile ni mashahidi ya jambo hili.

MAHUBIRI YA AINA AINA

Mahubiri yanayoendelea nchini 'Mapenzi ya Mungu' lilichangia kiasi cha kutosha. Yawe mahubiri moja kwa moja kwa kuchapisha au kuripori taarifa ya mijadala na mihadhara.

Kama wasomaji wote wanakumbuka kwamba tulikuwa na mjadala wa wiki kadhaa na Waislamu wa eneo la Kurasini, tulikuwa tukienda msikitini mwao kila wiki siku ya Jumamosi na hao ndugu walikuwa wakija msikitini mwetu Mnazimmoja, kesho yake siku ya Jumapili. Ndugu Waahmadiyyah wengi, wazee kwa vijana kwa shauku kubwa walikuwa wakihudhuria mahubirini. Hatimaye wakalazimika kutangaza kwamba Waahmadiyyah hawana kazi nyingine isipokuwa kuhubiri tu. Kwa hiyo hawawezi kuendelea kujadiliana nasi. MAPENZI YA MUNGU liliendelea kuarifu wasomaji taarifa yote ya mjadala ule. Nakumbuka kwamba katika mazingira hayo ndugu yangu Bwana Mahmudu Hamsini Mubiru akasema kwamba "Sasa Waahmadiyyah waweza kutembea mjini kifua mbele."

UHUSIANO MZURI KWA SEREKALI

Katika miaka ya 1999 hadi 2002 uhusiano mzuri sana ukajengeka baina ya Serekali ya Mwungano wa Tanzania na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah. Katika historia ya Jumuiya mara ya kwanza kabisa Viongozi wa ngazi ya juu kabisa ya Serekali walianza kuhudhuria mikutanoni mwetu na kuisifu Jumuiya hadharani, kama Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, Waziri wa mambo ya ndani, Waziri wa ofisi ya Waziri Mkuu na Mkuu wa Polisi. Ilihali zamani Viongozi wa Serekali za Mikoa tu walikuwa wakihudhuria Mikutanoni mwetu.

BARUA ZA PONGEZI

Vile vile Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu walianza kuandika barua rasmi kwa niaba yao na kwa niaba ya Serikali yao kumtakia Khalifa Mtukufu kila la heri, hongera na mafanikio mazuri ya Mkutano wa Mwaka wa Uingereza. Taarifa hizi zote zilitolewa na MAPENZI YA MUNGU zilizosababisha mahubiri kote kote nchini.

Ilimuradi Gazeti la MAPENZI YA MUNGU ndiyo mbinu kubwa ya mahubiri na malezi vile vile. Mwenyezi Mungu Atusaidie kutangaza Neno la Lake kote kote kwa juhudi yote bila hofu yoyote, ili bishara ya Ufunuo wa Seyyidna Ahmad a.s. Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah,itimie isemayo: " Mimi nitafikisha Ujumbe na mahubiri yako kwenye kila pembe ya Dunia."

muzaffardurrani@yahoo.com
muzaffardurrani@gmail.com

Wanajumuiya ya Ahmadiyya walioshiriki katika harakati za uhuru

Kutoka uk. 1

na kadhalikaa. Pia ilihusika na uhuru wa Tanganyika. Jitihada kubwa zilifanywa na wafuasi na hata viongozi wa Jamaat hii kuhakikisha kuwa uhuru unapatikana. Ndiyo maana tunaona kuwa katika kundi la wakuu wa kwanza wa iliyokuwa mikoa ya Tanganyika asilimia 20 ilikuwa ni Waahmadiyya.

CHIFU MOHAMMED KALUFYA (MFADHILI WA TANU).

Ingawa kuna sababu nyingine zitolewazo juu ya kwa nini Tanganyika ilikuwa ni nchi ya kwanza kupata uhuru wake, lakini sababu moja kuu na ya muhimu mno huwa haitajwi nayo ni hii kwamba Mwalimu Juliasi K. Nyerere aliwashika sana machifu ambao walikuwa wakitiiwa na kuheshimika sana na watu wao. Nao ni kama vile Mkwawa wa Iringa, Gabrieli Ruhumbika wa Ukerewe, Fundikira wa Tabora, Nyarubamba Kianja (Bukoba), Mwami Thereza Ntare (Biharamulo), Makongoro wa Ikizu (Musoma) Kidaha Makwaiya wa Kahama, Chifu Mazengo, Chifu Majebere Masanja, Chifu Dastan Ngua, Chifu Erasto Mangeya, Humbi Ziota na kadhalika.

Katika orodha hiyo ya machifu yupo Ahmadiyya mmoja aliyeitwa Mohamed Kalufya, huyu alikuwa ni chifu wa kabila la Watongwe.

Huyu alizaliwa mwaka1889 na kufariki tarehe 5, Desemba, 1982 huko uvinza mkoani Kigoma. Mzee Kalufya alikuwa ni mchapakazi wa kuigwa kwani mnamo mwaka 1952 ingawa alikuwa ni chifu, lakini alishinda zawadi ya Mkulima Bora wa mwaka wajimbo la Magharibi (Western Province).

Chifu Kalufya ambaye Ikulu yake ilikuwa katika wilaya ya Mpanda Mashariki mahala ambapo ndipo palipokuwa kitovu cha vuguvugu la siasa. Chifu Kalufya allikuwa miongoni mwa waasisi wa TANU mwaka 1954. Yeye aliitumikia TANU vilivyo. Na alitoa wakfu nyumba yake iliyoko Mishamo kwa chama cha TANU. Nayo baadaye ilifanywa kuwa ndiyo ofisi ya wilaya ya chama cha TANU.

Uadilifu wa mzee huyu uliwashawishi watu wengi katika wilaya ya Mpanda wakajiunga na TANU na Watongwe wengi walipata nguvu ya kujiunga na harakati za uhuru, baada ya kuona kuwa TANU imepokelewa vyema na Chifu wao.

Viongozi wengi wa kisiasa walikuwa wakimtembelea sana Chifu Kalufya ili kupata ushauri wake. Watu kama Musa Rehani, Saidi Maswanya, Rajabu Tambwe ni miongoni mwa watu mashuhuri ambao walikuwa hawakosekani katika Ikulu ya Chifu Kalufya. Hata baada ya uchifu kufutwa na Serikali, bado Chifu Kalufya aliendelea kuwatumikia watu wake kama kiongozi wa Jadi. Alihamasisha mno kilimo na kuhubiri umoja baina ya watu. Chifu Kalufya aliaminiwa sana katika kutoa maamuzi. alitumia sana hoja zilizomo katika tafsiri ya Qur'an Tukufu iliyotolewa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya mnamo mwaka 1953.

Tarehe 5 Desemba, 1982 Chifu Kalufya alifariki dunia na kuacha pengo kubwa kwa kabila la Watongwe, Jumuiya ya Ahmadiyya na jamii ya wapigania uhuru.

ABDALLAH AHMAD MARUNDA (Shujaa wa vita vya Majimaji).

Bwana Abdallah Ahmad Marunda alizaliwa katika kijiji cha Mchotike tarafa ya Njinjo Kilwa mnamo mwaka 1891. Huyu alikuwa ni Imamu wa Msikiti wa Ngongowele.

Historia inaonyesha kuwa vita vya Majimaji vilikuwa ndiyo chemchem ya mapambano ya uhuru, yaani chimbuko la mapigano ya uhuru lilijengwa na vita vya Majimaji. Basi Abdallah Ahmad Marunda alishiriki vita vya Majimaji akiwa kijana mwenye umri wa miaka 14. Yeye alikuwa na mtu aliyependa uhuru wake. Na kwa hivi alipohudhuria kwenye vikao vya akina Kinjeketile Ngwale waliokuwa wakipinga ujio wa Wakoloni wa Kijerumani na kuishawishi jamii kufanya vita vya kufa na kupona kuiokoa nchi isitwaliwe. Abdallah Ahmad Marunda aliamua kujitolea kushiriki vita hivyo. Kuna rawaya isemayo kwamba vita vya Majimaji vilianzishwa



Mzee Abdallah Ahmad Marunda

na Waislamu kupinga ujio wa watawala ambao waliwaita "Balya ligulube" (wala nguruwe).

Abdallah Ahmad Marunda ambaye kaka yake Hemedi Ahmad Marunda ndiye aliyeleta Qur'an Tukufu katika Kilwa ya Bara. Kaka yake alifariki mwaka 1908 na mwaka 1909 alifiwa na baba yake, mwaka 1911 alikataa wito wa kwenda kujifunza uchawi. Mnamo mwaka 1914 Mkuu wa Wilaya wa Kijerumani alifika Kilwa kuomba vijana wajitolee kwenda kupigana katika vita vikuu. Bwana Marunda alimshauri Bwana Mkuu wa Wilaya kuwa mtu ni vigumu kujitolea mwenyewe bali yeye ateue tu. Ndipo Bwana Mkuu wa Wilaya alipomteua Marunda kuwa kama kiongozi na kisha kuwachagua vijana wengine.

Bwana Marunda alishiriki vita kuu vya kwanza vya dunia tangu mwaka 1914 mpaka 1918. Na kuanzia wakati huo Bwana Marunda alihesabiwa kuwa kama ndiye kiongozi wa Wamwera wa Njinjo.

Bwana Marunda alikuwa mtu aliyependa ukweli na hakuacha kupokea mabadiliko yoyote yalipojiri. Ndiyo maana ilipofikia wakati wa kudai uhuru yeye hakuingia katika siasa kutokana na kutoa mno muda wake katika shughuli za dini, lakini alikuwa akiwahimiza watu kwamba wasirudi nyuma,bali waunge mkono harakati za uhuru. Miongoni mwa vijana waliokuwa karibu sana na Marunda, alikuwa ni Bwana Saidi Mohamedi Manoro ambaye baadaye alikuja kuwa katibu mkuu wa kwanza wa chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA).

Historia ya upinzani wa Bwana Marunda dhidi ya Ukoloni ni ndefu, kwani hata alipokuwa jeshini katika vita kuu vya kwanza vya dunia, mara kadhaa aliwahi kukorofishana na maafisa wa Kijerumani waliokuwa wakionyesha dharau kwa Waafrika. Hata siku moja aliwahi kuelekezewa bastola na mtunza ghala wa Kijerumani na Bwana Marunda hakuwacha kutetea Waafrika bali alitamka "ALLAHU AKBAR" kwa kishindo. Yule mtunza ghala wa Kijerumani aliponyokwa na ile bastola yake. Na baada ya siku chache mzungu yule alifariki dunia. Jambo hilo lilimfanya Bwana Marunda siyo aheshimiwe tu bali hata kuogopwa.

Bwana Marunda Alijiunga na Ahmadiyya mwaka 1957 kwa kuhubiriwa na mpwa wake, Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima. Bwana Abdallah Ahmad Marunda alifariki tarehe tarehe 22 Agosti,1974 na akazikwa Temeke Dar es Dar es Salaam kwenye makaburi ya Ahmadiyya.

HASSAN TAUFIQ. SULEMANI (baba wa Harakati za Uhuru).

Hassan Taufiq Sulemani ndiye mtu anayedhaniwa na kuwa ndiye baba wa Harakati za Uhuru wa Tanganyika. Mzee huyu ambaye mnamo mwaka 1925 yeye alikuwa mwanafunzi wa darasa la sita katika shule ya St. Andrew College, Minaki Kisarawe, Dar es Salaam. Alizaliwa tarehe 5 Septemba, 1912 katika kitongoji kilicho umbali wa maili 25 kutoka Dodoma mjini kiitwacho Msanga. Baba yake Taufiq Hassan alizaliwa Unguja na wazazi wahamiaji waliotoka Masasi. Shughuli za uchuuzi zilimfikisha Taufiq Hassan katika jimbo la Kati (yaani mkoa wa Dodoma). Hassan Taufiq ndiye mtu ambaye aliweza kuwashawishi watu wengi hasa wasomi wa Makerere Kampala, Uganda kujiunga na chama cha TAA (yaani Tanganyika African Association). TAA kilikuwa ni kama cha kijamii ambacho chini kwa chini kilifanya kazi ya siasa.

Kuna wakati TAA ilikuwa Dar es Salaam tu. Ni Hassan Taufiq ndiye ambaye kwa gharama zake alisafiri na kuieneza TAA Tabora, Bukoba, Kigoma, Mbeya, Arusha, Mwanza na mikoa mingine mingi. Wakati huo Mwenyekiti wa TAA alikuwa ni Bwana Ali Ponda, ambaye pia alikuwa ni Mwalimu wa Hassan Taufiq. Tanga mwaka 1933 Bwana Hassan Taufiq alikuwa Karani katika Idara ya Mifugo huko Dodoma.

Mwaka 1941 Mwalimu Ali Ponda alipewa uhamisho kwenda Ihema na nyuma yake Bwana Hassan Taufiq ndiye aliyekuwa mkuu wa TAA katika Dodoma. Nafasi hii ilimfanya kuwa mtu muhimu sana wa wakati huo katika siasa ya Tanganyika.

Ni wakati huo ndipo Bwana Hassan Taufiq alipoweza kuwasiliana na kuwa karibu sana na wanaharakati wa uhuru wa sehemu mbalimbali nje ya Tanganyika. Kwa mfano ni katika miaka hiyo ndipo alipokuwa akiandikiana na Bwana George Padmore aliyekuwa gwiji la siasa za muunganowa weusi, vuguvugu ambalo zama hizo lilijulikana kama Pan-Africanism.

Bwana Hassan Taufiq ambaye alifahamiana sana na Mwalimu Juliasi K. Nyerere ndiye aliyefungua tawi la kwanza la TANU jimboni Dodoma. Yeye ndiye alikuwa katibu wa kwanza na Bwana Ali Ponda akawa Mwenyekiti wake.

Ili kuonyesha kwamba yeye hakuwa mwenye haja ya madaraka ya kisiasa. Baada ya uhuru alijweka mbali na shughuli za kisiasa. Bila shaka Bwana Hassan Taufiq Suleimani ni mmoja wa watu ambao uhuru wa Tanganyika ni matunda yao. Huyu ndiye Bwana Hassan Taufiq ambaye alikuwa ni Myao aliyeunganisha makabila mbalimbali ambaye aliamini sana juu ya kauli mbiu ya TAA "Umoja na Nguvu" ambayo baadaye ilirithiwa na TANU.

MTEMI KOMAGI AHMAD SANSA MGALAGANZA

Ahmad Sansa alikuwa ni mmoja wa Watemi. Yeye alikuwa mtoto wa Sultani wa dola ya Ngalanganza hupo Usaguzi Tabora. Mama yake alifariki miezi miwili baada ya kuzaliwa mtemi Komagi. Ahmad Sansa alizaliwa mwaka 1908 na alifiwa na baba yake mnamo tarehe 28 Januari, 1922, na hapo yeye akatawazwa kuwa mfalme wa dola ya Ngalaganza. Raia wake walimpeleka shule ya Utawala wa Wazalendo, Home School, Kizigo Tabora.

Naye pia alikuwa ni miongoni mwa waasisi wa TANU na alijiunga siku ileile chama kilipoanzishwa mnano mwaka 1954. Tangu mwaka huo hadi alipofariki mwaka 1958 aliendelea kutumikia chamacha TANU ambacho alikipenda kwa sababu ya kudumisha heshima ya Watanganyika.

Mwaka 1958 Mtemi Ahmad Sansa alikuwa miongoni mwa wakaribishaji katika mkuano mkuu na wakihistoria uliofanywa na TANU. Ulio maarufu kwa jina la Azimio la Tabora. Sansa pia alikuwa mjumbe wa kikao hicho muhimu ambacho hadi leo historia inatuonyesha kwamba mkutano huo ulikuwa na ajenda muhimu mno katika mipango ya uhuru wetu. Inasemwa kwamba kilikuwa kikao cha kujadili mada ya kura tatu. Jambo lililokuwa likielekea kuleta mtafaruku katika chama.

Mgogoro huu ulitatuliwa kutokanana suluhisho lililotolewa na Mbashiri wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanganyika Sheikh Inayatullah U. Ahmad Chaudry. Ahmad Sansa pia alikuwa mshairi mashuhuri wa Kiswahili nchini. Mashairi yake yalisomwa sana katika magazeti ya Mambo Leo,Mkola Sizwe, Baragumu, Tazama la Kenya, Mapenzi ya Mungu na kadhalika. Na idadi kubwa ya masharii yake yalikuwa ni kuhusu wito wa mapambano ya uhuru.

Endelea uk. 8

Tafsiri ya Kurani Tukufu na harakati za uhuru

Kutoka uk. 3

Magharibi tunaona jinsi gani wafanyakazi wanavyonyonywa na mabepari na haki za akina mama zinavyopuuzwa. Lakini islam iliyarekebisha maovu hayo karne nyingi zilizopita.

Ukweli ni kwamba Kurani Tukufu imehubiri uhuru kamili na usawa na imemuweka binadamu kwenye kilele cha uhuru. Katika aya zilizoteremshwa mwanzo mwanzo zinasema:

"Lakini hakufuata njia ya Aqabah (mlimani).

Na nini kitakujulisha njia ya Aqabah ni nini.

Ni kumpa mtumwa uungwana. (90:12-14).

Kazi nzito ya kupanda mlima ambao binadamu alikuwa bado hajajitahidi kutekeleza ilieleza kuwa ndio njia ya utakaso, kilele cha wema na kila Mwislamu lazima ajiwekee shabaha hiyo na kuitekeleza ambayo ni kumpa uhuru mtumwa.

UKOMBOZI KUTOKA MIUNGU BANDIA

Hatua zilizochukuliwa na Kurani Tukufu katika kumkomboa binadamu ni hizi zifuatazo:

(1)

Kurani Tukufu ilimkomboa binadamu kutoka kwa miungu bandia na ikamfanya yeye kutawala kila kitu hapa duniani. Binadamu ambao kabla ya hapo walikuwa wanaabudu jua, mwezi, moto, maji, miti, sasa wakaanza kuwa watawala wa vitu hivyo. Kurani Tukufu ilipandisha heshima ya binadamu kiasi hiki ya kwamba sio tu binadamu alitawala viumbe vingine bali hata malaika walitakiwa wamsujudie na kila kitu kilicho mbinguni na ardhini kilitakiwa kumtumikia.

(2) Usawa wa binadamu:

Kurani Tukufu inatangza kuwa bindamu wote waliumbwa na Mwenyezi Mungu na wote wanachimbuka kutokana na shina moja. Kwa kufanya hivyo ikafuta mipaka ya utaifa, ukabila, itikadi na ile imani ya kuwa wapo walio bora kuliko wengine na ikateketeza tikitiki mizizi yote na matawi ya utumwa. Watu wote inasema Kurani Tukufu, wawe matajiri au maskini wawe weupe au weusi, wa Mashariki au Magharibi wote wanatokana na asili moja, hivyo wote wana haki sawa. Inasema Kurani Tukufu:

Enyi watu! mcheni Mola wenu ambaye Amewaumbeni kutoka katika nafsi moja, na Ameumba kutoka katika nafsi ile nafsi yenzie, , na kutoka katika nafsi hizo mbili Akaeneza wanaume wengi na wanawake; na Mcheni Yeye bilkhususi kwa kuziheshimu fungamano za kidugu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu. (4:2)



Sheikh Waseem Ahmad Cheema aliyewahi kuwa Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania akimkabidhi hayati Mwl. J. K. Nyerere nakala ya Tafsiri ya Kurani Tukufu.

Kwa njia hii Kurani Tukufu inasimamisha na inalinda uhuru, usawa na haki za kila bindamu, ikitambua kuwa wote wamechimbuka kutoka shina moja bila shaka ilimsaidia binadamu wakati wake wa shida akielewa kuwa kwa kufanya hivyo anamtumikia Mwenyezi Mungu. Hivyo Mwenyezi Mungu amempendelea sana binadamu kwani kwa kumtumikia unakuwa umemtumikia Mwenyezi Mungu. msaada huo unahesabiwa kuwa ni ibada.

3. Chimbiko Moja.

Kurani Tukufu inaeleza undugu wa binadamu wote kuumbwa na Mungu mmoja na imeeleza undugu wa damu, lakini Kurani Tukufu imetambua uhusiano huu wa aina mbili. Haijali sana tofauti za kabila na koo isipokuwa inatambua kwamba sote tunatokana na Adam na Hawa. Hivyo hapana nafasi ya mtu mweupe kujiona yeye ni bora kuliko mweusi wala mweusi kujiona bora kuliko mweupe. Kurani Tukufu imewaleta watu wote pamoja na kutangaza:

Enyi watu! kwa hakika Tumewaumbeni katika kiume na kike, na Tumewafanyeni mataifa na makabila ili mjuane; hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye zaidi katika ninyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari. (49:14)

Tofauti pekee sawa na aya hii ni Taqwa (ucha Mungu). Mtu anayefuata amri za Mwenyezi Mungu na kuwatendea wema viumbe wa Allah ni hivyo hivyo anapanda madaraja. Kwa hiyo sawa na Islam watu wote ni huru na sawa, mbora ni yile anaye mcha Mwenyezi Mungu zaidi na nafasi hiyo iko wazi kwa kila mmoja kuipigania.

4. Kukata minyororo ya kutawaliwa

Siku zote mabepari wamejitahidi kuwasaga tikitiki wafanyakazi. Wafanyakazi kabla ya Islam walikuwa na hali mbaya kuliko watumwa. Minyororo ya riba iliwafunga wasiweze kutoka. Kurani Tukufu ikatangaza kuwa riba ni haramu, hivyo ikamkomboa mfanyakazi kutoka kwenye makucha ya Mabepari ambao siku zote wanakusanya bila kujali kuwapa wafanyakazi haki yao kabla jasho lao halijakauka. Miaka mingi kabla hajazaliwa Karl Marx Kurani Tukufu ilikuwa tayari inapigania haki za wafanyakazi na ukombozi wa kweli ni ukombozi wa kiuchumi.

5. Chimbiko la Utawala:

Kabla ya Islam, wafalme na watawala walijiona miungu watu! Neno lao lilikuwa sheria. Kwa upande wake Kurani Tukufu inasisitiza kwamba madaraka yanatakiwa wapewe wale wanaostahili. Watawala na watawaliwa ni sawa mbele ya sheria. Juu ya Serkali gani inafaa, Kurani Tukufu inasema ya kuwa utawala lazima utokane katika kushauriana na ridhaa ya watu. Na huo ndio msingi wa demokrasia au kama alivyosema Abraham Lincoln aliyekuwa rais wa Marekani, Serkali ya watu, inayoendeshwa na watu, kwa faida ya watu. Juu ya uongozi, Kurani Tukufu inasema madaraka ni amana na wapewe wale wanaostahiki yaani wanaoweza kuibeba na kuitekelezea amana hiyo haki zake. Viongozi wa kweli ni watumishi sio mabwana. Kama anavyosema Mtume Mtukufu s.a.w "Bwana wa kaumu ni yule anayewatumikia". Sheikh Kaluta Amri Abedi kwa kulielewa hilo naye akaimba:

Ujaliwapo makamu
cheo wakakutunuku
umeshikishwa khatamu
Za punda mwenye shabuka

Nawe jifanye Ghulamu
Kama mtumwa sumbuka
Kuwakhudumu kaumu
Khuduma ya kutukuka.

utawala wa fikra:

Kabla ya Islam viongozi wa dini na wasomi walikuwa wanatawala fikra za watu na walitaka wafuatwe bila ya kuuliza. Kuuliza lilikuwa kosa. Islam ikaondoa utumwa huu na kufundisha kwamba mtu yupo huru kuuliza na kutofautiana na wengine katika swala la mawazo. Mtukufu Mtume Muhamamd s.a.w. alisema: Kutofautiana kwa maulmaa wangu ni neema".

Ubovu wa Mila

Baadhi ya Mila hazifai. Islam inasema sio lazima mila hizo zifuatwe iwapo watu ambao walionekana kulaaniwa katika jamii. Kwa mfano huko Nigeria katika kabila la Waibo walikuwepo Waosu. Wanawake walikuwa hawaruhusiwi kula mayai na watoto mapacha walitupwa kwani walionekana kuwa ni balaa katika jamii. Mila hizi ziliwanyima uhuru na haki zao za msingi. Islam inauliza swali la msingi nyinyi mnawafuata mwenendo wa wazazi wenu hata kama walikuwa hawajui?

Udhaifu wa kijinsia:

Lilikuwa pingamizi kubwa katika dhana ya uhuru. Wanawakendiowalioumiazaidi katika mfumo dume uliotawala dunia. Uarabuni ilikuwa ni siku ya huzuni anapozaliwa mtoto wa kike ndani ya familia. Baadhi walidiriki hata kuwazika wangali hai. Hali ya mwanamke haikuwa bora kuliko ya mtumwa. Hakuridhi, wala ridhaa yake haikutakiwa katika ndoa. Lakini islam ilileta ukombozi uliokamilika kwa mwanamke. Ruhusa ya kuridhia kwao katika ndoa imetolewa, bali ndoa haikamiliki bila ya ridhaa ya mwanamke. Wanawake wakaweza kushiriki katika kila nyanja ya maisha hata kwenye vita vya jihadi. Katika Islam, ikafundishwa kwamba nusu ya elimu ya dini itapatikana kwa mama wa waaminio, bibi Aisha r.a. Alipoulizwa ni nani anastahili kutendewa wema zaidi miongoni mwa watu, Mtume s.a.w. alijibu, Mama yako, kisha mama yako, kisha mama yako, kisha baba yako!! Hii inaonesha cheo alichopewa mama katika Islam. Umuhimu huo umesisitizwa zaidi kwa kauli ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. aliposema: "Pepo ipo chini ya nyayo za akina mama". Juu ya ridhaa ya ndoa Sheikh Kaluta Amri Abedi anaielezea kwa ufasaha:

Ndoa pasipo wazazi, kuridhi haiafiki,
Si ndoa ni upuuzi, katu hatuisadiki,
Na binti naye hawezi kuozwa kama hataki.

Ubaguzi wa rangi:

Mengi yametokea duniani kutokana na rangi. Binadamu wamebaguana na kudhrauliana kutokana na rangi zao. Ni ajabu mtu anawezaje kuringa na kujiona kwa kitu ambacho alipewa bure bila ya kufanya jitihada yoyote. Shaabani Robert anafafanua vizuri kazi ya rangi aliposema:

Rangi pambo lake Mungu, rangi haina kashifa,
Ni wamoja walimwengu, wa chapati na wamofa,
Walaji ngano na dengu, wazima na wenye kufa
Rangi pambo lake Mungu si alama ya maafa.

Kurani Tukufu inafuta dhana hii potofu kwa kusema, tumeumbwa makabila na mataifa mbalimbali ili tujuane tu lakini mbora wetu ni yule anayemcha Mungu zaidi. Mfano mzuri ni wa Hadhrat Bilal r.a. aliyekuwa swahab wa Mtume s.a.w anayeheshimika sana ingawaje alikuwa mweusi – Mhabeshi. Kurani Tukufu inasema: Bila shaka Tulimwumba mtu kwa umbo bora. Binadamu ameumbwa kwa umbo bora, sio Mhindi, Mchina, Mjapani, Mzungu, Mwarabu au Mwafrika bali binadamu. Hapawezi kuwepo na tangazo bora la uhuru kuliko hilo. Kwa ujumla hiyo ndiyo Falsa ya Islam ambayo Sheikh Mubarak Ahmad alipopewa fursa ya kufundisha kule Tabora na Sheikh Abdul Karim Sharma aliyekuwa rafiki mkubwa ya Julius K, Nyerere alimtembelea mara kwa mara Mwalimu Nyerere huko shule ya Mtakatifu Francis Pugu na kumuelezea Falsafa hizo za Islam. Ni dhahiri ukisoma hotuba za Nyerere, maandiko ya TANU na hatimaye CCM yanadhihirisha athari iliyopatikana kutokana na mafundisho hayo ya Islam kama yalivyofafanuliwa na maulamaa wa Jumuiya ya Ahmadiyya.

Mwisho

Bustani ya Washairi

Mashairi

MASHAIRINAHARAKATIZA UHURU

Upo ushahidi wa kutosha wa kuonesha jinsi gani mashairi yalivyosaidia harakati za uhuru. Akina Saadan Abdul Kandoro, Ahmad Sansa n.k. walitunga mashairi yaliyohamasisha umma wa wakulima na wafanyakazi. Fani hiyo ilitumiwa vilivyo na Sheikh Kaluta Amri Abedi alipotafsiri hotuba ya Mwalimu Nyerere kutoka Kiingereza kuja Kiswahili. Katika hotuba hiyo KILIO CHA UHURU aliweka ubeti ambao ni wito wa ukombozi, ubeti huo ni: Sauti iliyoshuka, kutoka ng'ambo ya nyota
Yanadi Waafrika, utumwa watautoka,
Yasema na Tanganyika, Mkitaka kuipata,
Njia ni kuunganika, katika chama cha TANU.

NDOVU AKAVWIRA WIMA

Hili ni shairi linalodhaniwa kuwa ndilo la kiswahili zaidi katika mashairi ya kisasa ya kiswahili.
Ukiondoa labda Al - Inkishafi, Rasil - ghuli na Diwani ya Muyaka. Basi shairi hili ndilo linalochukua nafasi ya kuwa na sifa ya ushairi wa kiswahili.
Inasemwa kwamba Mwalimu Julius K. Nyerere alilitundika shairi hili ofisini kwake (Ikulu) na alikuwa akilikariri kila asubuhi.
Shairi hili lilitungwa na Sheikh Kaluta Amri Abedi (r.a) wakati wa harakati za kudai uhuru chambilicho ni kwamba shairi hili lilihusika na kuzirudi karaa na shutuma zilitolewa na wakuu wa wilaya enzi hizo, ambao walitoa matukano makubwa dhidi ya Rais wa TANU Mwl. J.K.Nyerere na chama chake kwamba ni chama cha wahuni na wavunja amani.
Ndiyo maana katika ubeti mmoja mtunzi anadai kuwa "kuja apite nyenyere, kazua nyamtitima".

Hapa anaonyesha kwamba watu wakubwa enzi hizo walikuwa wakihutubu na kufanya mikutano mikubwa lakini hawakulaumiwa, ila Nyerere ambaye ni mtu mdogo, ukilinganisha na serikali ya wakoloni yeye ni kama nyenyere tu alipozungumza alishutumiwa na watu wa serilali.
Kwa hivi Sheikh Kaluta alitunga shairi ili kuhamasisha waafrika washikamane, kuanzia Tanganyika, Mvita hadi Unguja waunganishe nguvu kuwatimua wakoloni ambao kwa mabavu yao ya utawala aliwafananisha na ndovu.

1. Mambo ya kale na leo, pindi ukiyatizama,
   Kwa juu maogeleo, au kwa mbizi kuzama,
   Ni ajabu kumbweneo, panda za mti kwachama,
   Ndovu akavwira wima, sisimizi akakwama!

2. Tobo lilivyaa tata, na tembe ilisakama,
   Tangayikana mvita jikumbateni matama,
   Na unguja nawaita panda za mti kwachama,
   Ndovu akavwira wima, sisimizi akakwama!

3. Mwanambiji mzingile, zinguo ni makarama,
   Vyambile zilungupule, vyawataka mahukama,
   Msambe kitukumile, panda za mti kwachama,
   Ndovu akawira wima, sisimizi akakwama!

4. Tambo ni hii yatamba, tambueni maulama,
   Kuitoa mkizimba, si kuimba lelemama,
   Si uto wa kuku temba, panda za mti kwachama,
   Ndovu akawira wima, sisimizi akakwama!

5. Ajabu ndovu avwire, pasi jani kutetema,
   Kuja apite nyenyere, kazua nyamtitima,
   Wakashangaa ngedere, panda za mti kwachama,
   Ndovu akawira wima, sisimizi akakwama!

6. Iwapo umfunguzi, fungulia kilokwama,
   Uwapo ni mchukuzi, zigo hili kwa likwama,
   Ufumbue ufumbuzi, panda za mti kwachama,
   Ndovu akawira wima, sisimizi akakwama!

7. Saba hizi abuyati, atangaze kiloloma,
   Atilietashititi, zijibiwe na ulama,
   Kisa cha panda za mti, panda zilizoachana,
   Ndovu akawira wima, sisimizi akakwama!

Sheikh Kaluta Amri Abedi

TANGANYIKA MPYA

1. Nashukuru Mola, Mwenye baraka,
   Mwingi wa fadhila, Na kutukuka,
   Kaziviza hila, Zimefutika,
   Ije Tanganyika, Kujitawala.

2. Hila zilipangwa, Tubaki nyuma,
   Hali ya kuwingwa, Kama wanyama,
   Tukawa wafungwa, Nchi nzima,
   Wasio heshima, Wala fadhila.

3. Tulikaguliwa, Kwa kila jambo,
   Vyema vikiliwa, Twala makombo,
   Au kusaziwa, Kuosha vyombo,
   Na kunuka shombo, Na nyingi dhila,

4. Tulifanya kazi, Na za harubu,
   Pasipo majazi, Yalo wajibu,
   Tukawa matwazi, Wenye kulabu,
   Au mabawabu, Wasio lala.

5. Tungawa wapole, Walitudhili,
   Tukasotwa ndole, Za ufedhuli,
   Zikatupa ndwele, Zao kauli,
   Tukaitwa nduli, Kupewa ila,

6. Tukaomba dua, Baadhi yetu,
   Akazichukua, Muumba wetu,
   Ndipo tukazuwa, Umoja wetu,
   Wakakiri watu, Kila kabila,

7. Tukazuwa TANU, Kwa shangwe nyingi,
   Kwa wali wa vyanu, Wenye mashungi,
   Ndipo kina nunu, Kina kiyungi,
   Wakaja kwa wingi, Kwenye shamala.

8. Jambo la uhuru, Tukawambia,
   Lataka kukuru, Fedha kutia,
   Utumwa kufuru, Kisha udhia,
   Tuzikaze nia, Kujitawala

9. Nao waasia, Pia wazungu
   Wote ni raia, Katupa Mungu,
   Tutaangalia, Wasile chungu,
   Tuwape kafungu, Ka utawala.

10. Ndipo nchi yetu, Ikazinduka,
    Kila pembe watu, Kuunganika,
    Na Nyerere wetu, Akasumbuka,
    Tukamuitika, Sote holela,

11. Kani akatia, Mwana Nyerere,
    Na Jonh Rupia, Naye Kihere,
    Na tulosalia, Kama tetere,
    Tukaimba shere, za utawala.

12. Shere tukacheza, Na mkoloni,
    Akivugumiza, Twabanda chini,
    Akitukonyeza, Hatuamini,
    Tukashika kani, Kujitawala,

13. Mpya Tanganyika, Inatokeza,
    Tumeunganika, Tumependeza,
    Waasia wetu, Na wangereza,
    Tutawaongoza, Kwa utawala.

14. Mataifa yote, Twende pamoja,
    Hakuna chochote, Cha kutufuja,
    Twapendana sote, Bila mauja,
    Imetimu hoja, Ya kutawala

15. Tushukuru Mungu, Watanganyika,
    Kupenya mizungu, Na mishabuka,
    Na kila ukungu, Ukafutika,
    Na nyota kutoka, Ya kutawala.

Sheikh Amri Abedi

UHURU JAMBO HALISI

1. Tundu liwe la dhahabu, la lulu na alimasi,
   Litiliwe abuwabu, kwa mbao za abunusi,
   Ndege huona adhabu, kuwekwamo mahabusi,
   Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

2. Uhuru ni mawahibu, katoa Mola Mkwasi,
   Pamwe na kuukutubu, uenee kwa unasi,
   Uhuru jambo wajibu, kwa ajinani na insi,
   Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

3. Kwa tunu watughilibu, wapate kutufilisi,
   Tudumu na ubawabu, nao washike urasi,
   Tuzidi kuwatulubu, kwa kazi za piga pasi,
   Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

4. Utumwa haujaghibu, bado waenda kwa kasi,
   Mwenye nguvu anasubu, mnyonge hana nafasi,
   Ukisema una tabu, wazidishiwa tatasi,
   Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

5. Vya bure vyao vitabu, wao haviwatakasi,
   Wamevipangia babu, kuupumbaza unasi,
   Na usawa umeghibu, hata ndani ya kanisi,
   Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

6. Na ufanye la harubu, u mweusi, u mweusi!
   Kamwe hulipwi thawabu, sawa na aso mweusi,
   Wewe zako ni sulubu, kuwakhudumu wakwasi,
   Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

6. Dharau zinatusibu, kudharawiwa Weusi,
   Maponjoro hutujibu, kwa maneno ya matusi,
   Asili ya hii taabu, ni kwamba tu mahabusi,
   Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

7. Nchi hii mahabubu, haki ni nchi ya sisi,
   Vile kuwapa karibu, sisi tumekuwa fisi,
   Sasa ni kheri kilabu, wapendwa kuliko sisi,
   Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

8. Kutawaliwa labibu, mtu hukui upesi,
   Yako mema maarubu, hayaachiwi nafasi,
   Watapenda uwe bubu, wakunyonye kipapasi,
   Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

9. Mwenyeji kuwa gharibu, huu dhahiri mkosi,
   Na jingine la ajabu, ni woga wetu wa fisi,
   Jambo latustahabu, tuunganike upesi,
   Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

10. Iko siku kwa Wahabu, sisi tutakuwa sisi,
    Hapo hatutawasubu, kwa dhiki na wasiwasi,
    Japo wanatuharibu, hatutawapa tatasi,
    Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Sheikh Amri Abedi

UHURU WA TANGANYIKA

1. Hai mambo hai mambo, Mola katakabalia,
   Yamekamilika mambo, uhuru umetokea,
   Hapanapo baya jambo, haja zimeshatimia,
   Sote twaushangilia, uhuru wa Tanganyika.

2. Mambo yalo kuwa kombo, yameshatuongokea,
   Natuushike mtambo, nchi tukijijengea.
   Leo sisi hatujambo, hapanepo la udhia.
   Sote twaushangilia, uhuru wa Tanganyika.

3. Furaha ya hili jambo, leo twalihadithia.
   Tutayafanya mpambo, kuadhimisha ulua,
   Hata watokao ng'ambo, tambo waje itambua,
   Sote twaushangilia, uhuru wa Tanganyika.

4. Nakishi zenye urembo, sisi tutajipambia,
   Tulipige la mgambo, dunia itangazia,
   Furaha yote majimbo, Tanganyika fahamia,
   Sote twaushangilia, uhuru wa Tanganyika

Endelea uk. 7

Kutoka uk. 6

5. Tutachgua warembo, zawadi kututwalia,
Wampe shumbe na Robo, uhuru alotetea.
Na dua zisyende kombo, mkimbozi mfikia.
Sote twaushangilia, uhuru wa Tanganyika.

6. Kazi kubwa ndio jambo, usoni linatwijia,
Kujenga nchi kiyambo, mambo yataendela,
Tukome kula makimbo, nao wale yetu pia,
Sote twaushangilia, uhuru wa Tanganyika.

7. Shime tuzipige tambo, wengine wajilalia.
Waamkapo tung'ambo, nyuma tumewaachia,
Hili kaagiza Babo, Nyerere mwanangu kua,
Sote twaushangilia, uhuru wa Tanganyika.

8. Kaditamatio mwimbo, na mwimbo umetimia
Lishamiri jema jambo, vema kujiangalia
Waungwana hatujambo, tudumishe uhuria
Sote twaushangilia, uhuru wa Tanganyika
Komagi Ahmad Sansa

UHURU UWE WA KHERI

1. Kwa Mola twatawakali, Bwana mwenye Amri,
Mungu chukua kabuli, ombi la hili shairi,
Tutokwe na udhalili, utubariki Kahari,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

2. Uwezo unao Jalali, wa kutukinga na shari.
Teupukwe na thakili, walaili wanahari
Yetu ardhilihali, Tanganyika iwe shwari
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

3. Tufarijike rijali, na nisai kuwa kheri,
Barakazo tusabili, nasi tuone fahari,
Shangwe yetu bilkuli, iwe njema ya johari.
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

4. Majuto situkabili, Tanganyika inawiri,
Tupate hiki kibali, tuitimize nadhiri,
Ombi nchi yetu jamili, Tanganyika kuwa huri.
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

5. Uhuru umewasili, pasipokuwa na dosari
Kwa upole na sahali, kwa madai ya saburi
Hakikuzuka kitali, kupigana kwa hanjari
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

6. Nyerere siye mkali, kama wale majeuri,
Na hiyo siyo kauli, ya siasa ya kiburi,
Amefaulu kamili, kwa kudai kimahiri
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

7. Pasizuke mushikeli, wa mizozo na kikiri,
Wageni kupokwa mali, maisha kuwa hatari,
Huo ni ubaradhuli, ni kujipalia nari,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

8. Tusijivune muhali, viburi tusishamiri,
Kufoka kama fahali, tujidai mahodari
Ya heshima tuyajali, tutakuwa mashuhuri.
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

9. Pasizuke mikatili, kama Kongo kukithiri,
Kujifanya majahili, mpole kuwa kufari,
Haitakuwa halali, tulinde yetu nadhari
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

10. Tuepushie ajali, za kupondwa na magari,
Taabu za kila hali, yafaa tujihadhari,
Kauli tusibadili, yakazuka machachari
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

11. Tuwe wenye akili, tuwasifu Mawaziri,
Ambao walihimili, kuiongoza safari,
Sifa wanastahili, bahari walivinjari
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

12. Tama naona dalili, tutafaulu dahari,
Mambo yamekuwa kweli, na leo ni dhahiri
Imeundwa serikali, ya Matumbi imejiri.
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Mathias Mnyampala - Penda Chako

KIVULI CHA RAHMANI

1. Twakushukuru Taala, Mola wetu wa mbinguni,
Kutufikisha mahala, mahala hapa nchini,
Kwa muda wa utawala, aruba wa zaidani,
Kivuli cha Rahmani, mtawala alo mwema.

2. Mtawala alomwema, kivuli cha Rahmani,
Hufurahika Karima, kwa tamko la Amini,
Ndipo nchi ikavuma, watini wa zaituni,
Kivuli cha Rahmani, mtawala alo mwema.

3. Ilikuwa Tanganyika, zama zile Wakoloni,
Nchi ilisalitika, tukawa hatujuani,
Na kodi inapofika, watu kamba viuononi,
Kivuli cha Rahmani, mtawala alo mwema.

4. Nimezaliwa Ujiji, ya Kigoma mkowani,
Wazee kina Kajiji, waliwekwa utumwani,
Wakubwa kuwafariji, kuwabeba mabegani,
Kivuli cha Rahmani, mtawala alo mwema.

5. Nalazimika kusita, kutaja ya Wakoloni,
Yalopita yamepita, tumwachie Manani,
Mkombozi akafika, Nyerere mwana chuoni,
Kivuli cha Rahmani, mtawala alo mwema.

6. Kwa juhudi za Mwalimu, Nyerere mwana chuoni.
Bendera yetu adhimu, ikafika kileleni,
Kambarage muadhamu, akawa wetu rubani,
Kivuli cha Rahmani, mtawala alo mwema.

7. Nchi zetu muungano, wa bara na visiwani,
Wakashikana mikono, Juliasi na amani,
Mkubwa mshikamano, wasangaa wapinzani,
Kivuli cha Rahmani, mtawala alo mwema.

8. Chonde chonde viongozi, mlio madarakani,
Vitazameni vizazi, vilioko vijijini,
Ndiko kwenye nguvu kazi, ishibishayo mijini,
Kivuli cha Rahmani, mtawala alo mwema.

9. Ewe Mola mwenye enzi, twakuomba ya Dayani,
Mwongoza viongozi, hakuna chako kifani,
Tung'arishie Azizi, nuruyo mwetu mwilini,
Kivuli cha Rahmani, mtawala alo mwema.

Kainuza H.R. Mbambwa (Wa Ujiji),
S.L.P. 90136,
Magomeni, Dar es Salaam.

ZAMANI HIZI NI ZAMA

1 Bismillahi Manani, jina lako Allahuma,
Mwandiko wangu auni, ndanimwe muwe hekima,
Shairi lisiasini, libebe mawazo mema,
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

2. Kwenu ninyi waumini, ninyi hao mahukama,
Ndooni mtathmini, haya ninotakalama,
Kama yana walakini, nyiye mtakujasema,
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

3. Mliyopita vyuwoni, mliketi kwa kusoma,
Naomba nielezeni, vitabu vinavyosema,
Zile sahifa za dini, wengine ni maamuma,
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

4. Samai na ardhini, kila janibu kwavuma,
Matukio duniyani, yanavyoata alama,
Kila moja ni ilani, kuna kitu huko nyuma.
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

5. Vyema hauonekani, mwezi tukiutazama,
Kwa vifaa na kwa mboni, nuru yake inazima,
Hii kubwa kulikoni, mashekhe nini mwasema,
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

6. Juwa na mwezi katwani, kukutana huko sama,
Kumbe kwa sababu gani, sasa haya kuandama?
Katikati pana nini, elezeni maulama!
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

7. Oleni juu mbinguni, mambo yanavyotutuma,
Mvuwa hunyesha porini, Allah tini Anatuma,
Ifikapo ardhini hufurika tunazama!
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

8. Ndege zawapo hewani, zinaruka na kukwima,
Zinatiwa matatani, hulipuka na kutoma,
Watu waliyomo ndani, wote hufa kama nyama!
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

9. Matetemeko yakini, mengi hayana ikama,
Yalikotukiya kwani, yamehilikisha uma,
Wengi hawaonekani, wamefukiwa kisima,
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

10. Ukimwi tuseme nini, unasumbuwa sakima,
Dawa haipatikani, wauwa ovyo kauma,
Hesabu mamilioni, kila mwaka wautema!
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

11. Ona hayapatikani, maakuli yamelema,
Kwao waliyo kazini, na hata kwa wakulima,
Ndaa tele duniyani, mwanadamu hajakoma!
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

12. Tazama umaluuni, utendwao na anima,
Himaya zinaidhini, sheria ya kuparama!
Waume wakitamani, kuowana si lawama!
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

13. Ndowa kadha maskini, za hivi tunazisoma,
Watu wema walaani, ruhusa ilo inama,
Haifikishi mbinguni, baraka tunajinyima,
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani,

14. Yanaashiriya nini, matukio yanovuma,
Yanaunguza moyoni, inasagika mitima,
Ewe Mola kuna nini, tu karibu na Kiyama?
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

15. Rejea wanazuwoni, ni ninyi mliyosoma,
Pekuweni mabukuni, ni nyingi mliyosoma,
Kwahiyo tafadhalini, nijuwe yalonilema,
Zama hizi ni zama, zama hizi zama gani.

16. Mashekhe nawaiteni, kwanza Ame muadhama,
Sauti nyembamba ndani, na **Simba dume** simama
Mniambiye yakini, zama gani hizi zama,
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

17. 'Kungwi' upo walakini? Haya njoo ujesema,
Na Mbambwa wa Magomeni, 'Akili Si mali pima,
Ninyi mnasema nini, zama gani hizi zama.
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

18. Mahmood Hamsini, na 'Wingi si Hoja' thuma,
Mikila Moro.mjini, na Kisusa uje hima,
Taali mnipasheni, zama gani hizi zama,
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

19. Kwako 'Mpenda Amani' waTandahimba chechema,
Na Bundala liwatani, jitokeze kwa kalima,
Mkadaru Musa - Pwani, wazijuwa hizi zama?
Zama hizi ni zama, zama hizi zama ani.

20. Tama mwisho wa kughani, muuliza maamuma,
Ninyi mnaobaini, nipeni kitu kizima,
Bayana niambiyeni, pahitajika salama,
Zamani hizi ni zama, zama hizi zama gani.

Al-Ustadh Khamisi S.S. Wamwera,
Kimbangulile - Mbagala Rangi Tatu,
Kata ya Charambe, Dar es Salaam

Mashairi juu ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara pamoja na miaka 75 ya Gazeti la Mapenzi ya Mungu bado yanapokelewa na yatawekwa katika matoleo yajayo. Inshallah. Mhariri

MZEE SULTAN UNGANDO - Ahmadiyya shupavu, chimbuko la kuanzishwa makao ya Kitonga.

Na Ussi Mohamed Ussi
Dar-es- Salaam.

Miongoni mwa wazee shupavu wanaoitetea, kuitangaza na kuindeleza Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ni Mzee Sultani Mohamed Ungando.

Akiwa ni msomi mwenye ufahamu wa elimu ya kizungu na ile ya kidini, Mzee Sultani Ungando alizaliwa mwaka 1924 katika kijiji cha Mbuchi, Tarafa ya Mbwera Wilaya ya Rufiji Mkoa wa Pwani.

Alianza kufundishwa kusoma Qur'an na baba yake ambae alifariki mwaka 1934. Baadae alijiendeleza kwa mwalimu Ally Mlanzi, na kasha kuhamia Kiongoroni kwa mwalimu Jabir Adam Marombwa.

Mwaka 1942, alianza elimu yake ya kizungu katika shule ya N.A. School iliyoko Muhoro Wilayani Rufiji. Mwaka 1947 hadi 1950 alisoma Shule ya boding iliyopo Utete Wilayani Rufiji na mjini Dar es Salaam.

Mwaka 1951 alijiunga na shule ya Ufundi ya Ifunda mjini Iringa, alisoma hapo kwa miaka minne na mwaka 1955 alianza kazi mjini Lindi kwenye Kampuni ya Tom Garage.



Pamoja na uchovu wa uzee na ugonjwa, Mzee Sultani Ungando (aliyefumba macho) anaonekana akiwa katikati ya Wanajumuiya wengine katika moja ya mikutano ya Jalsa Salana inayoendelea kufanyika huko Kitonga nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Mwaka 1956 alikuja mjini Dar es Salaam na kujiunga na Kampuni ya Coper Motor Co-operation(CMC), akiwa fundi mkuu na baadae akawa msimamizi. Mwaka 1991 alistaafu kufanya kazi na kuamua kuwa mkulima hadi hii leo.

Alijiunga na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya mwaka 1956 chini ya Mbashiri Mkuu wa wakati huo Sheikh Abdul Karim Sharma. Sababu iliyomfanya ajiunge na Ahmadiyya, ilikuwa ni baada ya kusoma gazeti moja la wakati huo liitwalo East African Standard.

Ilikuwa ni mwaka 1952, ndani ya maktaba ya shule ya Ifunda wakati wakati yeye akilisoma gazeti hilo. Ndani ya gazeti kulikuwa na habari iliyoeleza kupatikana kwa Tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa lugha ya Kiswahili juzuu zote 30 na sura 114 iliyoandikwa na Sheikh Mubarak Ahmad.

Alijisikia furaha sana kuona kwamba sasa Tafsiri ya Qur'an imeandikwa na Waislam wenyewe tofauti na ile iliyoandikwa na Padre Dalle amabyo ilijaa makosa mengi na kudhalilisha Uislam. Habari hiyo njema aliwaambia rafiki zake Ally Mgunda na Masoud Abdallah Msolome.

Aliporejea nyumbani wakati wa likizo, aliwaeleza wazee wa huko kuhusu habari ya kupatikana tafsiri ya Qur'an Tukufu. Wao walimtisha na kumwambia akae nayo mbali kabisa tafsiri hiyo ya makadiani.

Lakini yeye hakutishika na maneno hayo , akiwa mjini Lindi mwaka 1955, alinunua msahafu wenye tafsiri hiyo toka kwa Sheikh Ahmad Mataka au "busra" kwa bei ya sh.30. Msahafu ambao hapo awali ulinunuliwa na muumini mmoja wa kisuni na baadae kuurudisha kwa madai kuwa tafsiri hiyo ya makadiani. Na msahafu huu Mzee Ungando anao hadi hii leo kama kumbukumbu yake.

Mwaka 1958, alifunga ndoa na binti wa Ahmadiyya ambaye ni Mzee Mussa Seif Sungu Matimbwa wa Nyipala Lusende Rufiji. Amejaaliwa kupata nae watoto wanne , wawili ni wa kike na wawili wakiume.

Wakati Bw. Mahamoud Hamsini Mubiru alipotoa wazo la kutafuta eneo la kujenga shule, Mzee Sultani Ungando alisema yeye analo eneo na yuko tayari kulitoa. Amir Sahib alielezwa habari hiyo, na akaagiza likaangaliwe eneo hilo kuona kama linafaa.

Ujumbe uliokwenda kuangalia eneo ulileta majibu kuwa ni eneo zuri na linafaa kwa maendeleo ya Jumuiya. Ndipo Mzee Sultan Ungando kwa kushirikiana na mkewe pamoja na watoto walijitolea eneo lao la ekari tano kuikabidhi Jumuiya.

Hilo ndio likawa chimbuko la Jumuiya kupata na maeneo mengine sehemu hiyo ya kitonga, ambapo sasa shughuli zote za Jamaat kama vile mikutano ya Jalsa, Shura, Ijtimai na sala za Iddi zinafanyika hapo. Hivyo kuondokana kabisa na ile adha iliyokuwepo hapo awali ya kukodisha sehemu kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za Jamaat. Mwisho.

Wanajumuiya na uhuru

Kutoka uk. 4

Ahmad Sansa ambaye kishairi alijiita kama "Komagi Mgalaganza" alifariki tarehe 6 Oktoba, 1966.

KALUMBA MOHAMED SALUM HASSAN KUNGULILO

Alikuwa maarufu kwa jina la Al-Haj Kungulilo. Asili yake ni Mluhingo wa Rufiji, lakini alizaliwa Tabora mnamo mwaka 1928. Baba yake alikuwa ni Mzee Salimu Hassan Kungulilo aliyekuwa mfasiri wa Kijerumani na mma yake aliitwa Maua binti Fundi aliyekuwa na asili ya Rwanda.

Huyu naye alikuwa ni miongoni mwa wanachama waanzilishi wa TANU mwaka 1954. Al-Haji Kungulilo alikuwa Katibu Mkuu wa kwanza wa Umoja wa Vijana wa TANU, yaani (TANU Youth League). Kabla ya hapo aliwahi kuwa makamu wa kwanza wa Rais wa Chama cha wafanyakazi nchini T.F.L. (yaani Tanganyika Federation of Labour). mwaka 1957 hadi mwaka 1959.



Alhajj Salum Hassan Kungulilo, aliyewahi pia kuwa Naibu Amir wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania

Al-Haji Kungulilo alikuwa na makomredi wenzake kama vile Rashidi Mfaume Kawawa, Abubakar Hassan, Kanyama Chiume, Kassim Baina na kadhalika. Na pamoja nao alishiriki sana katika kampeni za uhuru. Mzee huyu alikuwa ni mtu mwenye huruma sana kwa watu, ingawa yeye katika zama hizo alikuwa ni miongoni mwa watu wachache wenye elimu na kipato cha kutosha, alikuwa na kwa sababu ya kufurahia maisha, lakini hakuridhika kuona jinsi Waafrika wenzake walivyo kuwa wakinyanyaswa na Wakoloni na hivi akaamua kutumia kila uwezo alio nao ili kuisaidia jamii.

Ndiyo maana inashangaza kuona kwamba mtu kama Al-Haji Kungulilo ambaye alishika sehemu mbalimbali za uongozi katika serikali na mashirika ya Uma. Lakini kamwe hakujilimbikizia mali. Yeye aliamini katika elimu na hata urithi alioona unafaa kuwaachia wanawe ni elimu. Bali Bwana Kungulilo alisomesha hata ambao hawakuwa wanawe.

Huyu ndiye Kalumba (dagaa nene) Mohamed Salum Hassan Kungulilo, mtu mkweli, shujaa na ambaye alikuwa miongoni mwa madiwani wa kwanza wakati wa uhuru katika kata ya Kariakoo.

Si hao tu katika Waahmadiyya waliochangia vilivyo katika uhuru wa Tanganyika, bali kuna kundi kubwa la Wanajumuiya Waahmadiyya ambao kwa namna mbalimbali walihusika na mapambano ya uhuru. wapo watu kama vile Abubakar Hassan, mwalimu alitemfundisha mbinu za kivita Samora Moses Machel ambaye baadaye aliikomboa Msumbiji na kuwa Rais wa kwanza. Abu Bakar Hassan ndiye kamanda wa kwanza wa polisi wa Mkoa wa Magharibi.Rashid Jumanne Abdallah ambaye alikuwa katika wa TANU wa jimbo la Morogoro kabla ya uhuru na baada ya uhuru akawa Mkuu wa kwanza wa mkoa wa Tanga. Na kadhalika.

Ndiyo maana tunasema kuwa wapigania uhuru wa Kiahmadiyya wako wengi na historia itaendelea kuwakumbuka. Hata kama magazeti na vyombo vingine vya habari vitasusa kuwatangaza Allah atawalipa zaidi katika Akhera. Amin.

Historia ya Jamaat Afrika Mashariki

Na Sheikh Waseem Ahmad Khan, Dar es Salaam

Mtume wetu Mtukufu (saw) alipoeleza habari za zama za mwisho, alisema "Wakati utaufikia umma wangu ambapo Uislam utabaki kwa jina tu na Kurani itabaki maneno tu, ndipo Mwenyezi Mungu Atamtuma Masihi na Mahdi Atakayesimamisha Uislam na mafundisho ya Kurani Tukufu duniani. (*Mishkaat Kitabul ilm Alfaslul thaalith*).

Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) mkazi wa kijiji kidogo kiitwacho Qadiyani nchini India alidai kwamba yeye ndiye Masihi yule aliyeahidiwa na Imam Mahdi aliyetabiriwa na Mtume Mtukufu Muhammad (saw). Yeye ametumwa na Mwenyezi Mungu ili ushindi wa dini tukufu ya Kiislam upatikane duniani na watu wa dunia nzima waje kujumuika chini ya bendera ya Mtume Muhammad (saw). Kwa kuwakusanya watu hawa chini ya bendera ya Islam, alianzisha Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya mnano mwaka 1889 mwezi wa Marchi tarehe 23 na siku ya kwanza watu wapatao arobaini walijiunga na Jumuiyya hii.

Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya alisema; "Mwenyezi Mungu Ameniarifu mara kwa mara ya kuwa Atanipa heshima nyingi na Ataieneza Jumuiyya hii duniani, na watu wa mataifa mbali mbali wataungana na Jumuiyya hii, na kila taifa litakunywa m aji kutoka chemchem hii, na Silsila hii itaongezeka na kuenea kote. Kutakuwa na vikwazo vingi na mitihani mingi lakini Mwenyezi Mungu Atayaondoa yote na kutimiza ahadi Yake. Mwenyezi Mungu Ameniambia kuwa; "Atakupa baraka nyingi mpaka Wafalme watatafuta baraka kutoka nguo zako. Basi enyi wasikilizaji! Sikieni na kumbukeni mambo hayo na tunzeni bishara hizo kwenye masanduku yenu, ni jambo la Mwenyezi Mungu litakalotimia siku moja". (Kitabu cha Seyidna Ahmad a.s kiitwacho 'Tajalliyate Ilahiya' Roohani Khazaain jalada 20).

Ndugu zanguni tuone mpango wa Mwenyezi Mungu mwenye shani ya ajabu kwamba mwanzilishi mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya aliposema hayo alikuwa mtu asiyejulikana kwa watu waliyopo nje ya nchi ya bara la Hindi. Maneno hayo hayawezi kusemwa na mtu yeyote isipokuwa awe na habari kutoka kwa Mwenyezi Mungu - Mjuzi wa mambo ya ghaibu. Kama Mwenyezi Mungu mwenyewe



Sheikh Waseem Ahmad Khan, Mbashiri wa Mkoa wa Dar es Salaam

Anavyosema 'AALIMUL GHAIBI FALAA YUDH' HIRU ALAA GHAIBIHII AHADAN ILLA MANIRTADHAA MIN RASUULI' - Yaani (Mwenyezi Mungu) Yu mjuzi wa ghaibu, na Hamdhihirishii yeyote mambo ya ghaibu ila kwa yule Anayemchagua kuwa Mtume wake. (Sura Al-Jinn 72:27-28).

Ndugu wasomi, Mwenyezi Mungu Akiyatimiza maneno ya mja Wake barabara kuwa ni shahada juu ya ukweli wake. Kwa sababu hasemi kutoka kwake bali anasema kama anavyoambiwa na Muumba wake. Najinsi Mwenyezi Mungu Anavyopanga mipango ya kumfanikisha inawashangaza wapinzani na kuwaacha katika bahari ya mshangao na butwaa. wapinzani wanaojaribu kumwangamiza yeye na hawairuhusu sauti yake itoke nje ya maskani yake. Lakini ni nani anayeweza kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu Mwenye ghera ya dini yake?

Ndugu wasomaji, kama nilivyosema kwamba mwanzilishi mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya alipodai kuwa Masihi na Mahdi wa umma huu wa Isalam na kusema na kueleza bishara mbalimbali za kuenea kwa Uislam duniani kwa kupitia Jumuiyya hii, alikuwa hana njia yoyote ya kufikisha ujumbe huu duniani, lakini Mwenyezi Mungu Aliyemtuma Alipanga mipango ya ajabu kabisa kwamba ujumbe ule kwa kutoka nje ya mipaka ya bara la Hindi ukafika nchi mbalimbali za dunia na watu wa mataifa mbalimbali na makabila mbalimbali wakaanza kukubali na kukusanyika chini ya mti huu wa kiroho uliopandwa na Mwenyezi Mungu Mwenyewe.

Bara la Afrika Mashariki ardhi ya Seyidna Hadhrat Bilal (ra) haikuwa nyuma bali ikafungua mikono yake ya kupokea ujumbe huu kama ilivyopokea wakati wa Mtume Muhammad (saw). Wakati ambapo Waislam walihama Makka na kuhamia Uhabeshi na kwa njia hii Uislam ulifika bara la Afrika Mashariki. Vile vile kwa kupitia wahamiaji watokao bara dogo la Hindi ujumbe wa kudhihirika kwa Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa ukafika bara la Afrika Mashariki. Yaliyotokea ni kwamba mnamo mwaka 1895, 1896 kutoka bara la Hindi baadhi ya watu walifika Afrika Mashariki wakitafuta kazi na wengine wakaletwa na wakoloni wakiwa wafanyakazi wa kutengeneza reli kutoka Kenya mpaka Uganda. Miongoni mwa hao walikuwamo wafuasi wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya, inasemekana kwamba Hadhrat Mirza Muhammad Afzal Sahib, Mhariri wa gazeti la Jumuiyya liitwalo 'Al-Badr' alikuwa mwanajumuiyya wa kwanza kufika Mombasa (Kenya) kutoka India.

Kulikuwa wengine waliofika katika miaka hii, miongoni mwao walikuwa akina Hadhrat Dr.Rehmat Ali, Hadhrat Dr. Faiz Ali, Hadhrat Sheikh Noor Ahmad, Hadhrat Dr. Muhammad Ismaili Guriani na Hadhrat Sheikh Hamid Ali Sahib.

Mnamo mwaka 1908 wanajumuiyya wa Afrika Mashariki walikuwa 60. Miongoni mwa hawa 12 walikuwa masahaba wa Seyidna Ahmad (as) na 48 walifanya Baiat kwa kumwandikia barua. (Sahaba ni yule aliyemwona Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa na kufanya Baiat juu ya mkono wake).

Hadhrat Dr. Muhammad Abdullah Khan Sahib aliyekuwa mhubiri mzuri alifanya mahubiri katika kabila la Memon. Kwa sababu ya mahubiri yake baadhi ya watu wa kabila hilo walijiunga na Jumuiyya. Watu hawa walipatikana katika kijiji cha Meru (Kenya).

Hadhrat Dr. Abdullah Khan Sahib alilazimika kwenda Tanganyika (Tanzania) kwa shughuli zake na kufanya mahubiri Tabora. Alikuwa mtu maarufu sana kutokana na tabia yake ya kufanya mahubiri mjini Tabora. Kwa kupitia njia hii ujumbe wa Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa ulifika Tanganyika (Tanzania).

Wakati ule nchi hizi za Afrika Mashariki zilikuwa chini ya utawala wa ukoloni na Wanajumuiyya walikuwa wametawanyika sehemu tofauti za bara la Afrika. Katika kipindi hiki waliendelea kufanya mahubiri na licha ya kuona upinzani waliendelea kuongezeka siku hadi siku mpaka mwaka wa 1934 ulifika, wakati ambapo katibu wa Mahubiri wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya Kenya Hadhrat Qazi Abdulsalaam sahib aliandika barua makao makuu na kueleza hali ya ukinzani uliopatikana mjini Nairobi dhidi ya Waahmadiyya. Aliandika "Hapa upinzani umepamba moto". Vipeperushi vyenye matusi na maneno ya kashfa vinapigwa chapa na kusambazwa dhidi yetu. Sisi kila wiki tunaandaa majibu na kuwapelekea watu. tumewaandikia wapinzani barua ya kufanya mjadala, waje kukubaliana masharti, upinzani umefanya kazi ya mbolea. Habari imeshamiri mjini na watu wenye tabia njema wanaelekea upande wetu. Kwa kupata taarifa hizo pamoja na ombi la Jumuiyya ya Nairobi Hadhrat Khalifatul Masihi wa Pili alimteua Sheikh Mubarak Ahmad Sahib akiwa Mbashiri wa kwanza wa Afrika Mashariki na kumwagiza aende Nairobi mara moja.

Sheikh Mubarak Ahmad Sahib alianza safari yake toka Qadiayani tarehe 11 Novemba 1934 na kwa njia ya meli alifika Mombasa mwishoni mwa Novemba na siku ya pili alifika Nairobi toka Mombasa kwa njia ya gari la moshi.

Kufika kwa Sheikh Mubarak Ahmad Sahib kulileta mafanikio mengi na Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya Nairobi ikaanza kuimarika zaidi na zaidi na Wanajumuiyya wakaanza kufanya mahubiri na kupanga mipango mbalimbali ya kufikisha ujumbe wa Jumuiyya. Upande mwingine upinzani ulizidi sana na wapinzani wakaanza kutumia hila kadhaa za kuimaliza Jumuiyya. Hila moja waliyoitumia ilikuwa kumwita Sheikh wao (Lal Hussein Akhtar) kutoka nchini India aliyekuwa maarufu katika kutumia maneno ya kashfa katika hotuba zake dhidi ya Jumuiyya. yeye alianza kutoa hotuba zenye matusi mjini Nairobi (Kenya) na kwa sababu ya hotuba zake upinzani ulipamba moto hapo.

Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya ilipanga mipango mingi ya kufikisha ujumbe, mathalani Mkutano Mkubwa juu ya sera ya Mtume Muhammad (saw) ulifanyika mjini Nairobi uliohudhuriwa na watu wengi.

Kwa kupitia mkutano huo watu waliweza kujua jinsi gani Waahmadiyya wanavyompenda Mtume Muhammad (saw). Mpango mwingine ulikuwa mjadala baina ya Sheikh Mubarak Ahmad Sahib na Sheikh Lal Hussein Akhtar uliofanyika mjini Nairobi tarehe 19 - 20 Januari 1935, siku ya Jumamosi na Juma pili. Mjadala huo ulifanyika juu ya mada tatu kuu na mada hizi zilikuwa (a) Kifo cha Nabii Isa a.s, (b) Utume unaendelea na (c) Ukweli wa Seyidna Ahmad a.s.

Watu waliohudhuria walikuwa takriban elfu nne. Miongoni mwa hawa walikuwa Waislam Waahmadiyya, Wasuni, Mabaniani na Masingasinga.

Katika mjadala huo Sheikh Lal Hussein Akhtar hakuweza kusimama mbele ya hoja za Kurani Tukufu zilizotolewa na Sheikh Mubarak Ahmad juu ya kila mada iliyojadiliwa. Sheikh Lal Hussein alijaribu kuwababaisha watu kwa kutumia ujanja wake lakini kila mara alishindwa mbele ya hoja za Kurani Tukufu. Mjadala huo ulifana sana.

Baada ya miezi mitatu Sheikh Lal Hussein mpinzani huyu wa Jumuiyya ya Mwenyezi Mungu alifukuzwa na watu wake na akalazimika kurudi India.

Endelea uk. 10

Dua za vilio silaha ya ukombozi Tanganyika

Kutoka uk. 12

(akiwemo aliyewahi kuwa Naibu Amiri wa Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania Alhaj Kalumba Hassan Mohammed Kungulilo ambaye pia alikuwa Naibu Mwenyekiti wa chama cha Wafanyakazi na Katibu Mkuu wa kwanza wa vijana wa TANU) vilifanya kazi nzuri ya kupigana bega kwa bega na chama cha Ukombozi TANU. Kazi hata hivyo ilipungua kidogo uzito wake kwa sababu Tanganyika haikuwa koloni ila ilikuwa chini ya udhamini wa Umoja wa Mataifa. Mara kwa mara ujumbe wa Umoja wa Mataifa ulikuja kukagua maendeleo ya nchi na aliyeongoza wazee wa Dar es Salaam ili kuonana na ujumbe wa umoja wa Mataifa alikuwa Mbashiri wa Ahmadiyya Sheikh kaluta Amri Abedi.

Habari zilikwenda vizuri kwani hapakuwepo na ubaguzi wa rangi, dini au kabila. Lugha ya Kiswahili na haiba ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere vikasaidia Tanganyika kuwa nchi ya kwanza Afrika Mashariki kujinyakulia uhuru. Wakati sasa tunashereheeka miaka 45 ya uhuru kuna haja ya kujiuliza ni sababu hizi tu zilizorahisisha kupatikana uhuru wa Tanganyika?

Wanahistoria wengi akina Kimambo, temu Othamn, Pratt, Rodney wamejikita zaidi katika sababu hizi tulizozitaja wakizinasibisha na kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika. Tunaziheshimu sana sababu hizo, lakini tunadhani tunaweza kwenda zaidi ya hapo.

Lipo jambo moja muhimu ambalo limejitokeza sana katika mapambano ya uhuru, na ni jambo la kusikitisha kuwa jambo hilo linatajwa kwa nadra. Jambo hilo ni maombi kwa Mwenyezi Mungu. Ukipitia historia ya mapambano utaona jambo hili linajitokeza sana. TANU ilipoanza tarehe 07-07-1954 ilianza kwa maombi. Mikutano yote ya TANU iliendelea kutawaliwa na utamaduni huu. Harakati za uhuru zilipopamba moto na wakoloni wakaonesha kuwa hawako tayari kutoa uhuru, Mwalimu Nyerere katika mkutano wa hadhara huko mjini Tabora alitamka "Mwisho wa yote tutamshitakia Mungu, maana yake kesi yetu tutaipeleka kwenye baraza la Muumbaji wa mbingu na ardhi, na bila shaka maana ya kupelekea kesi yako mbele ya mahakama ya mbingu si nyingine zaidi ya maombi. Matukio ya kufunga saumu ikiwa ni moja ya njia ya maombi ni mengi na lenye ushaidi mkubwa ni lile alilolitaja Mwalimu Nyerere mwenyewe alipokuwa Bagamoyo na akaomba maji amezee Aspro kwani kichwa kilikuwa kinamuuma kwa jili ya saumu. Jioni alipokwishapata chochote kichwa kilichokuwa kinamuuma kikapotea baidi! Licha ya chama cha TANU zipo baadhi ya Taasisi zilizoendesha sana maombi ili uhuru upatikane kwa amani na haraka.

Sheikh Mubarak Ahmad ambaye alifahamiana na viongozi wengi wa TANU wa wakati ule kwani alikutana nao Tabora alipokuwa anafundisha dini katika shule ya Tabora, anaeleza kuwa hakumbuki hata siku moja aliomwandikia barua Kiongozi wa Jumuiya ya Ahmadiyya ulimwenguni Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad r.a. bila ya kumuomba ili aiombee Tanganyika. Wanajumuiya hapa Tanganyika nao waliendelea kuomba ili uhuru upatikane kwa amani. Imani yetu ni kwamba Mwenyezi Mungu anatoa wito, "Niombeni nitawajibu" Hapana shaka moja ya sababu kubwa iliyouleta uhuru na kuendeleza amani tuliyonayo hivi sasa ni maombi yaliyofanywa kwa roho zilizo halisika kwani kama asemavyo mshairi mahiri wa Uingereza John Milton: "Mambo mengi yanaletwa na maombi kuliko tunavyofikiri. Utamaduni huu uliotuokoa huko nyuma tunao wajibu wa kuundeleza. Hapana mafanikio bila ya kumtanguliza Mwenyezi Mungu katika kila kitu. Ni faraja kuwa hata wimbo wetu wa taifa ni maombi na vikao vya bunge vinafunguliwa kwa maombi na viongozi wengi wanapenda kumaliza hotuba zao kwa kusema Mungu ibariki Tanzania. Ni kwa manufaa yetu kuuendeleza utamaduni huu kwani tumekwisha hakikishiwa na Mola Muumba kwamba: Niombeni nitawajibu na kila agongaye hufunguliwa.

Uhuru washerehekewa kwa dua

Kutoka uk. 12

akili mfano wa Mwalimu Nyerere. Aliongeza kwamba, kama viongozi wote wa Tanganyika na watu wengine wangefanya kazi pamoja kwa moyo wa dhati na jitihada, baraka za uhuru zingeendelea katika siku zote zijazo.

Shukrani nyingi zilitolewa kwa Jumuiya ya Ahmadiyya na Mwalimu Kihere wa Tanga ambaye ni mwanachama wa Bunge la Taifa kwa niaba ya wageni wote waliohudhuria kwa lengo la kuwatakia Watanganyika heri katika pato lao la kupata uhuru na kuwa na furaha, amani na mafanikio mema.

Jumuiya ya Ahmadiyya ya Tabora iliwakaribisha watu wengi pia katika karamu ya chai na kuwalisha maskini wengi na pia kuwapa zawadi watu mbalimbali kwa sura ya vitabu vya Kiislamu. Msikiti wa "Alfazal" na majumba yalipambwa kwa siku nne kwa taa za rangi mbalimbali kwa kusherehekea uhuru kamili wa Tanganyika.

Katika karamu ya chai Maofisa wengi wa Serikali walihudhuria kwa shangwe. Sheikh Inayat–Ullah alitoa hotuba fupi, akiwasihi watu waendelee kufanya kazi kwa furaha na Mapenzi ya Mungu aliyetupatia uhuru. Alisema kwamba kupata uhuru, kama Waziri Mkuu wetu alivyokuwa akisema, siyo shabaha yenyewe, kazi hasa imekwisha aanza sasa; na kama Kurani Tukufu isemavyo, Wale wanaomshukuru Mwenyezi Mungu, Yeye Huwazidishia neema zake.

Baada ya hotuba ya Sheikh iliyosikilizwa kwa makini sana, Bw. Jumanne Kombo, Katibu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya aliwapa wageni mashuhuri zawadi kadha wa kadha katika kusherehekea uhuru.

Mwenyekiti Bw. Tambwe, alipewa tafsiri ya Kiswahili ya Kurani Tukufu, katika hotuba yake ya kumaliza aliwashukuru wanachama kwa ajili ya zawadi hiyo na akasema kwa hakika Msahafu huo ulikuwa kitu cha kumfunua macho, ambao ungemzuia kupotoka wakati anapofanya kazi ya kuwatumikia watu wote kwa jumla.



Wakuu wa Mkoa wa mwanzo mara baada ya kuapishwa na Waziri Mkuu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Asilimia ishirini ya Wakuu hao wa Mikoa walikuwa Waahmadiyya. Mstari wa mbele wa pili kushoto ni Sheikh Kaluta A. Abedi, Mkuu wa Mkoa wa Tabora na wa kwanza kulia mstari wa nyuma ni Bw. Jumanne Rashid Abdallah Mkuu wa Mkoa wa Tanga.

Historia ya Jamaat Afrika Mashariki

Kutoka uk. 9

MPANGO WA KUCHAPA MAPENZI YA MUNGU.

Kwa fadhili na msaada wa Mwenyezi Mungu Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya iliweza kuchapa gazeti la dini liitwalo 'Mapenzi ya Mungu', gazeti ambalo mpaka leo linapigwa chapa na kuwawezesha wasomi wamalize kiu yao ya kiroho.

Katika toleo lake la kwanza Sheikh Mubarak Ahmad Sahib aliandika makala moja juu ya mada ya 'Mapenzi ya Mungu' kwa kumjibu Padri mmoja aliyeandika makala moja juu ya mada 'Raha kwa kafara' yaani wokovu unapatikana kwa kupitia kafara.

Sheikh Mubarak Ahmad Sahib alimjibu kwa kusema kuwa; "Wokovu unapatikana kwa sababu ya fadhila na mapenzi Yake (Allah)". Kwa njia hii gazeti hilo lilipewa jina la "MAPENZI YA MUNGU". Gazeti hili lilikuwa gazeti la pekee lililopigwa chapa kuitumikia dini tukufu ya Islam hapa Afrika Mashariki na mpaka leo linaendelea kutolewa na Jumuiyya. Katika uwanja huu wa elimu Jumuiyya ilikuwa mbele sana juu ya kuwaelimisha watu wa Afrika. Jumuiyya iliweza kuchapa vipeperushi vingi katika lugha ya kiswahili na Kiingereza na vitabu vingi juu ya mada mbalimbali.

Lakini kazi iliyojenga historia ya Jumuiyya hapa Afrika Mashariki ilikuwa kazi ya kutafsiri Kurani Tukufu kwa Kiswahili. Ni kazi iliyosifiwa sana na watu wote. Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya ilikuwa Jumuiyya ya kwanza iliyoweza kutafsiri Kurani Tukufu kwa Kiswahili. Ndugu msomaji ukipenda kusoma zaidi historia ya kazi hii basi nakuomba usome dibaji na kurasa za mwanzo za Tafsiri yetu.

Katika zama zile Tabora ilikuwa kituo kikubwa cha biashara nchini Tanganyika. Sheikh sahib alifika Tabora kwa ajili ya kufikisha ujumbe wa Jumuiyya. Ingawaje kabla hajafika yeye baadhi ya watu walikuwa wameshajiunga na Jumuiyya. Sheikh sahib alifika hapo na kuanza kupanga mpango wa kujenga Msikiti, na Msikiti wa kwanza wa Jumuiyya ulijengwa hapa nchini Tanganyika mwaka 1944, ambao ni maarufu kwa jina la Msikiti wa Fazl Tabora. Msikiti huu una historia yake pekee hapa Afrika Mashariki ambayo tutaiandika katika toleo lijalo Inshallah.

Sheikh Waseem Ahmad Khan - Mbashiri wa Mkoa wa Dar es salaam, Tanzania.

Mapenzi ya Mungu katika harakati za uhuru

Kutoka uk. 12

Washairi uk. 6 na7 wa gazeti hili).

Kwa upande wa siasa utafiti uliofanywa umeonesha ya kuwa gazeti hili toka TANU ianzishwe 1954, habari zake zilipewa heshima kwa kupewa nafasi kwenye ukurasa wa mbele huku ukioneshwa umuhimu wa TANU na harakati zake za kupigania uhuru. Hakuna mfano wa gazeti lililofanya kazi ya kueneza itikadi ya TANU kama lilivyofanya gazeti la Mapenzi ya Mungu. Gazeti la 'Mwafrika' lilikuja nyuma wakati mti wa uhuru ulikuwa umeshamea kwa kumwagiliwa mbolea kutoka Mapenzi ya Mungu. Gazeti hili lilitumia njia mbili kusambaza itikadi za TANU. Kwanza kupamba gazeti hili kwa vichwa vya habari vinavyosifia TANU na kutoa tahariri zinazohamasisha wananchi waishike vilivyo kamba ya ukombozi – TANU.
Mapenzi ya Mungu Vol. 22 Na. 5 la mwezi May 1959 lilikuwa na kichwa cha habari "amani ndiyo silaha ya TANU - asema Mheshimiwa nyerere.
Habari hiyo iliyoambatana na picha ya Mwalimu Nyerere ilisema. "Waandishi magazeti wawili waliotoka nchi za mbali walipomhoji Bw. Julius K. Nyerere juu ya uvumi wa kutokea machafuko nchini Tanganyika yeye aliwaambia ya kwamba hatazamii matata yoyote. Sisi tumekwishachagua silaha yetu ya kupigania uhuru. Silaha ile ni Amani na watu wetu wamekubali kuitumia. Hayo siyo maneno tuliyoanza kusema siku chache kabla ya Gavana kutoa tamko lake juu ya matengenezo nchini wala hatukusema vile kwa sababu maneno kama hayo yalihitajika, la, bali hayo ndiyo tulianza kuyatangaza tangu kubuniwa TANU miaka 5 iliyopita na tunyaamini kabisa."

Ili kutoa uzito zaidi juu ya silaha hii ambayo imeifanya Tanzania kuwa kisiwa cha amani hadi leo, tahriri ya Mapenzi ya Mungu katika gazeti hilo hilo (May 1959) ilisema "Maneno hayo kwa wakati ule yalikuwa ni ya kimapinduzi sana yenye dhamira ya kuhamasisha watanganyika waenzi amani". Ni jambo la kufurahisha kuwa somo hili la amani limeendelea kueleweka hadi hivi leo. Kama iko sifa inayotutofautisha na nchi nyingi zilizotuzunguka na zile zilizo mbali nasi basi ni hii hii ya kuenzi amani. Kama wanavyosisitiza Waswahili, ukiona vyaelea vimeundwa, basi na amani tuliyonayo imeundwa na bila shaka Mapenzi ya Mungu inayo nafasi maalum katika sanaa hii ya kueneza, kuirutubisha na kuihubiri amani.

Mapenzi ya Mungu la Oktoba 1959 Vol. 22 Na. 11 lilipambwa na kichwa cha habari "Bahati njema Tanganyika" Kichwa hicho cha habari kilitokana na tamko la Sheikh Kaluta Amri Abedi akieleza ya kuwa jukumu la kuwaelimisha wananchi lilikuwa ni la Serikali kwani wannchi wanatoa kodi. Sheikh Kaluta Amri Abedi aliilaumu Serikali iliyokuwa inawaambia Waislamu na wasio na dini kujenga shule zao badala ya kulalamikia shule za Misionari. Kuhusu hoja hiyo Sheikh Kaluta Alisema 'kumwambia mtu asiyejua kusoma aanzishe shule ni kumfanyia mzaha unaochusha'. Katika tamko hilo sheikh Kaluta alisema hakuna haki kwani shule za Misheni zilikuwa zinawachukua watoto wa Kikristo na kuwaacha wengine ilihali shule hizi zilikuwa zinapokea msaada kutoka serikalini, pesa zinazotokana na walipakodi Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Sheikh Kaluta alisifu sana uongozi wa TANU ambao ulikwisha iona kasoro hii. Mapenzi ya Mungu linaendelea kueleza kwa kumnukuu Sheikh Kaluta, "Hatari ya mpango huu wa elimu ulijulikana kwa viongozi wa TANU hata kabla ya AMNUT tarehe 4 Septemba 1957 Mheshimiwa bwana Julius K. Nyerere alitoa taarifa iliyotangazwa katika magazeti karibu yote ya nchi hii akilaumu mpango huu wa elimu, akaeleza wazi wazi ya kuwa hali hii haitakiwi katika nchi hii ya kwamba Waislamu wabakie nyuma ya Wakristo katika elimu".

Vikwazo vikubwa vya uhuru katika nchi nyingi za Afrika ilikuwa kuzusha uhasama wa dini. Uhasama huu ni mbegu mbaya na taifa huweza kuangamia. Sheikh Kaluta Amri Abedi kwa kupitia Mapenzi ya Mungu alitoa tahadhari juu ya hatari hii. Kwa kiwango kikubwa uhasama wa Waislamu na Wakristo ulidhibitiwa. Mapenzi ya Mungu mara kwa mara ilitoa mwito kwa watu kuheshimiana na kuvumiliana na kuwa mahubiri yanayofanyika yawe kwa njia ya hekima na busara, utamaduni huu bado unaendelea pamoja na kwamba huingia doa mara kwa mara.

Sera nyingne muhimu ya TANU ilikuwa ni kupigania uhuru na umoja wa bara la Afrika. Katika maandiko yake mengi TANU ilisisitiza juu ya uhuru na kuungana kwa nchi za Kiafrika. Kilio cha uhuru kilijitokeza sana katika gazeti la Mapenzi ya Mungu. Gazeti la Mapenzi ya Mungu la Februari 1960 vol 23 Na. 2, kichwa chake cha



Mwalimu J. K. Nyerere ambaye alikuwa mpenzi wa gazeti la Mapenzi ya Mungu katika msikiti wa Ahmadiyya Dar es Salaam.

habari kilikuwa ni "Upepo wa Mabadiliko wavuma Afrika". Hayo ni maneno yaliyotamkwa na Waziri Mkuu wa Uingereza Bwana Macmillan tarehe 3/2/1960 alipokuwa nahutubia huko Afrika Kusini. Maneno hayo yaligeuka kuwa mwiba mchungu katika bara la Afrika. Ni kweli upepo wa mabadiliko ulikuwa umeikumba Afrika kwani si muda mrefu Afrika nzima ilijipatia ukombozi. Nalo toleo la Mapenzi ya Mungu la mei 1960 likauliza swali muhimu, "Nyerere atakuwa Waziri Mkuu? Na lile la June 1960 likashangilia kwa kusema "Uhuru waja mbio Afrika".
Toka kianze chama cha TANU kilijikita katika kuwa sauti ya watu wanyonge, akina yakhe au maarufu baba kabwela, chama kilijijengea utamaduni wa kuwa watumishi na sio mabwana, sera hii ya kuwatumikia watu iliungwa mkono na Mapenzi ya Mungu na likatoa tahariri yenye utamu wa ajabu Februari 1960 iliyosema:
TANU ya Utumishi: Akitoa hotuba katika mkutano wa mwaka wa Chama
cha TANU tarehe 15 Januari, 1960, Rais wake ametamka maneno ambayo thamani yake haitapungua hata baada ya kupita miaka mingi: bali yatathaminiwa zaidi baadaye kuliko yalivyo sasa. Alisema kwa sauti kuu ya kuwa TANU ya kesho lazima iwe 'Tanu mpya- TANU ya utumishi'.
Watu wengi katika wanachama na viongozi wa TANU wanaona ndoto ya kupata cheo hiki au kile katika siku zijazo na ni wachache sana wanaofikiri ya kuwa baada ya uhuru
kupatikana nchini wanachama ndio watatakiwa kufanya kazi nyingi kuliko wanavyofanya hivi sasa kwa kuinua hali ya nchi na wananchi. Ni wazi ya kwamba kila mtu hawezi kuwa waziri au gavana au P.C. au D.C., la. Kwa hiyo yafaa watu wote ambao wanataka nchi ya Afrika itukuke zaidi machoni mwa watu wa ulimwengu mzima wajiweke tayari kwa utumishi wa kweli, ulio na uhalisi wa moyo na ambao unataka faida ya watu wote kwa jumla.
Jambo la pili alilosema Bwana Nyerere, ambalo ni muhimu kama lile la kwanza. ni kufanya uongozi wa TANU ukaribie 'uongozi wa dini', Maana yake, mawazo ya watu yasitangetange ovyo huku na huko, ball wawe na uongozi maalumu unaofuatwa siku zote kwa kila hali ya taabu na faraja. 'Tusiamini maneno tu kwa sababu Nyerere kasema. Jee, Nyerere akikanyagwa na motokaa kesho mtafanya nini?, aliuliza Rais mwenyewe alipokihutubu katika mkutano wa mwaka. Twaweza kusema kwa yakini ya kuwa ufaulu wa TANU umeletwa kwa sababu ya uongozi wake wa busara wa kumpa kila mtu anachostahiki pasipo kuangalia taifa lake, dini yake au rangi yake. Mtu ye yote anayetazama uongozi huo pasipo husuda atausifu. Baada ya kupata uhuru au baada ya kupata viongozi wa sasa ambao wanaelewa na kushika uongozi huo iwapo TANU itabadili uongozi wake na kushika njia ambayo ni kinyume cha uongozi wa sasa wa TANU, hapana shaka nguvu yake na umoja wake utapotea na nchi nzima itakuwa hatarini mpaka hapo ambapo chama kingine kitaundwa chenye uongozi wa haki.
Basi wakati huu yafaa kila mwenye tumaini la kuona nchi ya Tanganyika inaendelea aambiwe wazi wazi uongozi wa TANU ni nini na wanachama wanatakiwa kufanya nini. Baada ya kupata madaraka zaidi Watanganyika wakitikisika, dunia nzima itawacheka na kuwaita viongozi hao kwa majina mabaya. Tuna furaha kuona ya kuwa mpaka sasa viongozi wa TANU na wajumbe wao wanaosaidiwa na Bwana Nyerere wamefuata uongozi mwema wenye faida, Kinachotakiwa ni hii ya kwamba uongozi huu ufuatwe kwa bidii sana na watu wa mataifa yote wavutwe kufanya kazi kwa ajili ya faida ya jamii.

Nguzo hizo za TANU – amani, kubezwa kwa uhasama wa kidini, ukombozi wa bara la Afrika na viongozi kuwa watumishi na sio mabwana ni nguzo ambazo Mapenzi ya Mungu iliwakumbusha wananchi mara kwa mara na kwa kufanya hivyo likarahisisha kukubalika na kuungwa mkono na wnanachi wengi na hivyo kupatikana kwa uhuru tarehe 9 Disemba 1961. (Mwisho)

Mwl. Majid Sudi ametutoka



Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini imepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha Mwalimu Majid Sudi. ***Inna Lillahi wainnaa Ilayhi Rajiuun.***

Mwalimu Majid Sudi alifariki siku ya Jumatano tarehe 23/11/2011 na kuzikwa siku ya pili yake tarehe 24/11/2011. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Ampe ukaribu Naye Aiweke roho yake katika makazi yaliyotukuka. Amin.
Maelezo kamili juu ya maisha ya Mwl. Majid Sudi yatatolewa katika toleo lijalo Inshallah. Mhariri.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

Muharram 1433 AH | Disemba 2011 | Fatah 1390 HS

Toleo Maalum la miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara

Mapenzi ya Mungu katika harakati za uhuru

Gazeti la Mapenzi ya Mungu lilianzishwa mjini Tabora mwaka 1936 likiwa ni gazeti la kwanza nchini kuanzishwa na Waislamu. Sheikh Mubarak Ahmad, muanzilishi wa gazeti hili, alijiwekea malengo yafuatayo:

(a) Kuwaamsha Waafrika ambao walikuwa wanaonewa na kubughudhiwa kwa sababu ya rangi yao.

(b) Kujibu shutuma zilizotolewa dhidi ya mafundisho matukufu ya Islam kwa kuonesha ubora wa mafundisho hayo.

(c) Kutoa elimu kwa ujumla na hasa ya Uislamu ili kukamilisha utu wa mtu.

Kwa kiwango kikubwa malengo hayo yalifikiwa na ukapatikana ufaulu wa hali ya juu. Gazeti la Mapenzi ya Mungu limeendelea kuwa mwalimu mwenye hadhi yake likisubiriwa kwa hamu kila mwisho wa mwezi lilipotoka. Kutokana na maombi ya wasomaji wengi gazeti hili kwa hivi sasa linatoka mara mbili kwa mwezi.



Baadhi ya washairi maarufu nchini akiwemo Sheikh Amri Abedi, Matias Mnyampala, Hemed Feruz Mbiyana, Dr. Lyndon Harris na wengineo ambao walitumia gazeti la Mapenzi ya Mungu kama jukwaa la kupaza sauti yao ya kudai uhuru kwa njia ya mashairi

Sawa na malengo ya kuanzishwa kwake, gazeti la Mapenzi ya Mungu siku zote limekuwa mbele katika kuwaelimisha wananchi juu ya haki zao mbalimbali ikiwemo haki ya kuabudu sawa na imani yao bila ya kubughudhiwa wala kulazimishwa. Na kwa vile ili mtu aweze kuabudu sawa na utashi wake ni lazima awe huru, basi Mapenzi ya Mungu halikuwa nyuma kabisa katika kuona kwamba wananchi wa nchi hii wanajipatia uhuru wao kutoka mikono ya wakoloni.

Ili kufanikisha lengo hili, Mapenzi ya Mungu lilitumia nyanja mbalimbali zikiwemo za utamaduni, siasa, dini n.k.

Kwa upande wa utamaduni ambao ndio hasa kielelezo cha uhuru, Mapenzi ya Mungu limekuwa ukumbi wa washairi ambao waliona fahari kutoa mashairi yao kwani mhariri wa mashairi hayo alikuwa mwenzao Sheikh Kaluta Amri Abedi. (*Mfano wa mashairi hayo yamewekwa kwenye bustani ya*

Endelea uk. 11

Dua za vilio silaha ya ukombozi Tanganyika

Siri ya mafanikio, ambayo kwangu hutuka,
Ni kwa dua na vilio, machozi kutiririka,
Yakaumbwa matukio, na Mola wetu Rabuka,

Sheikh Kaluta Amri Abedi

Tarehe 09 Disemba 1961 saa sita na dakika moja usiku, bishara tukufu ilitimia Tanganyika. Mwenyezi Mungu ameahidi katika Kurani Tukufu kuwa analipa juhudi za anayejitahidi. Na ni dhahiri juhudi kubwa ilifanyika hadi bendera ya 'Unioun Jack' alama ya dola ambalo Winston Churchil alisema jua lake katu halitui, ikateremshwa kwa huzuni na unyonge mkubwa na kwa vigelegele na nderemo bendera ya alama ya taifa jipya nyeusi, kijani kibichi na manjano ikapepea mwanana ikitoa matumaini mapya. Safari yenyewe hata hivyo haikuwa sahali. Bahari ilichafuka, mawimbi yakawa makali, lakini chini ya nahodha wetu mahiri, chombo cha taifa letu kikatia nanga salama salimini.

Ni dhahiri shahiri jitihada kubwa ilifanyika. Abushiri, Mkwawa kwa kuwataja wachache wakacharuka na kunena 'haiswihi kutawaliwa' wakapigana. Mwaka 1905 bila ya kujali silaha za 'mkono wa damu' Wazalendo akiwemo Sheikh Abdallah Marunda, Mwanajumuiya wa Jumuiya Ahmadiyya Njinjo) walipambana na hao walowezi waliochukua ardhi, wakatoza kodi na kutandika watu viboko ndani ya ardhi yao. Vyama vya wakulima vikaanzishwa kupigania haki za wakulima. Vyama vya wafanyakazi

Endelea uk. 10

Uhuru washerehekewa kwa dua na shangwe

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya wa Tanganyika waliung'arisha na kuupamba msikiti na nyumba wakati wa sherehe za uhuru wa Tanganyika zilizofanyika tarehe 11 Desemba, 1961 katika "Masjid Salaam", Dar es Salaam. Sala nyingi ziliendeshwa na vitabu vingi vya Kiislamu viligawanywa bure.

Karamu nzuri iliyoandaliwa kwa kusherehekea Uhuru wa Tanganyika ilitayarishwa na Jumuiya ya Ahmadiyya ya Tanganyika. Msikiti uliangazwa kwa taa za rangi mbalimbali na kupambwa kwa bendera nyingi. Mkutano huu ulihudhuriwa na watu wengi kutoka sehemu mbalimbali za nchi miongoni mwao walikuwa wanachama wa National Assembly (Bunge la Taifa), viongozi wa TANU, Madiwani wa Dar es Salaam, Wakuu wa miji na wageni mashuhuri kama vile Waziri Mkuu wa British Guiana, Mjumbe Muhammad Saleh wa Chad na Meya wa Mansfield, Ohio.

Hotuba fupi zilitolewa kwa Kiswahili, Kiarabu, Kiurdu na Kiingereza na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Ahmadiyya Tanganyika Maulana Sheikh Muhammad Munawar ra, Mtaalamu A. Khalique, Maulana Sheikh Mubarak Ahmad, Amir Mkuu wa Jamia Ahmadiyya Sheikh Kaluta Amri Abedi na Sheikh Mussa Rehani wa Kigoma.

Wasemaji wote walionyesha furaha na kujivunia kwa kuzaliwa kwa taifa jipya la Tanganyika na kuwa nchi huru inayojitawala yenyewe.

Maulana Sheikh Mubarak Ahmad ra, alisema kwamba uhuru kama yalivyo mafundisho ya Kiislamu ni zawadi ya thamani kubwa sana kutoka kwa Mwenyezi Mungu na sasa ni juu ya watu wote wa Tanganyika kuitumia zawadi hii kwa fikira, werevu na shukurani kwa Mwenyezi Mungu ili kwamba taifa hili jipya liendelee kwa kupata mafanikio makubwa katika kuwatumikia watu. Alisema Tanganyika ina mfano mwema baina ya watu wa makabila mbalimbali walioungana pamoja ili kuifikia shabaha yao hii. Uhuru huu ungeweza kuwa na faida kubwa pia kwa nchi zilizo jirani.

Naye Sheikh Muhammad Munawar ra alisema kwamba Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu aliyetubariki kwa kutupa kiongozi mwenye

Endelea uk. 10